# BRELA

## WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

ISSN: 000401 | Toleo No. 07 | Septemba - Desemba, 2023




# USHIRIKIANO WA BRELA NA WADAU NI TIJA KATIKA UTENDAJI




brela_tanzania | BRELA Tanzania | brela_tanzania | +255 (0) 735 331 003 | BRELA ONLINE TV

# YALIYOMO


3 WALEENI WAFANYABIASHARA-DKT. KIJAJI



5 BRELA, TAKUKURU WAKUBALIANA KUHARAKISHA TARATIBU ZA UCHUNGUZI



17 KAMATI YA BUNGE YAIMWAGIA SIFA BRELA



34 NCHI WANACHAMA ARIPO ZATAKIWA KUONGEZA NGUVU KWENYE MILIKI UBUNIFU




BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY



*Bw. Godfrey Nyaisa*
*Afisa Mtendaji Mkuu BRELA*

# TAHARIRI

Nawakaribisha tena kwenye Toleo la Saba la Jarida letu la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Toleo hili limesheheni taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu na shughuli za urasimishaji biashara zinazotekelezwa kwa ufanisi na weledi wa hali ya juu.

Lengo letu ni kutoa elimu na kusambaza habari kwa umma kuhusu mambo yaliyotekelezwa na yaliyopangwa kutekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa BRELA wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026). Jitihada za makusudi za kuwawezesha wadau wetu kupata fursa ya kuelewa shughuli zinazofanywa na Taasisi yetu katika kuhakikisha huduma zinapatikana kwa urahisi, kwa ubora na kwa gharama nafuu zikiakisi Dira yetu ya kuwa Taasisi ya mfano katika utoaji wa huduma bora za usajili na utoaji wa leseni za biashara.

Taasisi inaendelea kuboresha mifumo ya utendaji kazi na kutoa huduma zenye ubora wa kiwango cha juu pamoja na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali katika kujenga mazingira wezeshi ya biashara nchini.

Tunatambua na kuthamini mchango wa kila mdau katika kufanikisha azma ya kuwa Taasisi ya mfano katika utoaji wa huduma bora za sajili za kibiashara, ulinzi wa miliki ubunifu kupitia usajili na utoaji wa leseni kwa kusogeza huduma karibu na wateja.

Ushirikiano na mashauriano ya mara kwa mara na wadau wa kimkakati kupitia vikao kazi na ushiriki katika matukio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa umekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha utekelezaji wa Mpango Mkakati na kuboresha taswira ya Taasisi kulingana na huduma zinavyotolewa kupitia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (ORS) na Dirisha la Taifa la Biashara (TNBP).

Kipekee tunawashukuru wadau wote walioitikia wito na kushiriki katika Maonesho ya kwanza ya Wiki ya Huduma za BRELA yaliyohitimishwa na Mkutano wa Mwaka wa Wadau uliofanyika Oktoba 27, 2023. Mkutano huo ulionesha mwelekeo mzuri katika kuendelea kuimarisha ushirikiano na ufanisi katika kutoa huduma bora na za uhakika.

Kwa ujumla Jarida hili, limebeba taarifa mbalimbali na makala za elimu na mafanikio ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika kipindi cha robo ya pili ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Taasisi yetu imezidi kung'ara katika utoaji wa huduma za sajili na Leseni pamoja na kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali ya wadau wakiwemo wawekezaji, wafanyabiashara na wanafunzi wa sekondari na vyuo mbalimbali nchini.

Aidha, Taasisi imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi pamoja na kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kupitia ushiriki katika mikutano, warsha, makongamano na semina mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa kwa ujumla.

BRELA inaendelea na jitihada za kuhamasisha na kuelimisha umma kupitia mitandao ya kijamii, makala na vipindi maalum vya televisheni/runinga na redio ili kuongeza uelewa miongoni mwa wananchi kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara, kusajili alama za biashara na huduma na kulinda vumbuzi zao.

Sambamba na hilo, wafanyabiashara wamekuwa wakikumbushwa kuhusu wajibu wao wa kuhuisha taarifa zao kwenye Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS), kuwasilisha mizania ya mwaka pamoja na taarifa za Wamiliki Manufaa, kuhusisha leseni za biashara na viwanda kwa wakati na kwa mujibu wa sheria.

Ninawatakia usomaji mwema na ninakaribisha maoni yenu ili kuboresha huduma zetu na uhusiano na jamii.

**BODI YA UHARIRI**

**Andrew Mkapa -** Mwenyekiti
**Roida Andusamile -** Katibu

**WAJUMBE**

Meinrad Rweyemamu
Tawi Kilumile
Abdul-rahman Twaha Songoro
Neema Kitala
Yusuph Nakapala
Tulizo Mpina
Alpha Nuhu

# Waleeni wafanyabiashara -Dkt. Kijaji

**Na Theresa Chilambo**

Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt Ashatu Kijaji ameitaka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kuwalea wafanyabiashara nchini kwa kurahisisha namna ya kuwafikia na kubuni mbinu za kuwahudumia ili kukidhi malengo ya kuanzishwa kwake.



*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akifungua Mkutano wa Wadau BRELA uliofanyika Mlimani City, Dar es Salaam.*

Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji alitoa rai hiyo wakati akifungua Mkutano wa Wadau wa BRELA uliofanyika tarehe 27 Oktoba, 2023 katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Alieleza kuwa kuanzia mwaka 2019 Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) kwa kuondoa tozo na kodi zaidi ya 374 katika sekta mbalimbali zilizokuwa zikiwasumbua wafanyabiashara.

Alisema mpaka sasa Serikali imefikia zaidi ya asilimia 75 ya kuondoa kodi hizo sumbufu.

Alisema Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 jumla ya Sheria na Kanuni 13 zimeweza kupunguza na kufuta tozo, ada na faini 67 ikiwa ni lengo la Serikali ya Awamu ya Sita la kuhakikisha mazingira ya biashara yanaboreshwa.

Waziri alisisitiza kuwa hakuna uchumi wa nchi unaokua kama hakuna maendeleo katika sekta za viwanda na biashara zilizo imara.



*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akiangalia bidhaa za mmoja wa wajasiriamali walioshiriki Maonesho ya BRELA yaliyofanyika katika viwanja vya Mlimani City, jijini Dar es Salaam.*

“Serikali inahakikisha inaboresha mazingira ya uanzishaji na ufanyaji biashara ndani na nje ya Tanzania na taasisi za udhibiti hazitumii mamlaka zao kufungia biashara yoyote lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa sekta ya biashara inalea uchumi wa nchi,” alisema.

Waziri alisema anatambua kuwa wafanyabiashara wapo mbele zaidi kwa kuwa dunia haiwezi “kutusubiri” na kwamba kwa kasi hiyo Wizara ya Viwanda na Biashara imeweka dhamira ya kuboresha Sera na Sheria ili zisomane na mabadiliko ya uchumi.

“Tunaangalia uwekezano wa kutoa leseni zote za biashara katika mfumo mmoja wa BRELA kuliko kuwa na mifumo mingi inayotoa huduma za leseni za biashara. Hii itasaidia uratibu mzuri wa leseni za biashara na

Serikali kuwa na kanzi data moja ya taarifa za biashara. Tunawaomba mtupe ushirikiano katika hatua hii ili tuwahudumie kwa ufanisi mzuri," aliongeza Mhe. Dkt. Kijaji.

Aliitaka BRELA kutumia mkutano huo na wadau wake kama jukwaa la kupokea maoni ya Watanzania, kuboresha na kutumia vema maoni hayo na kwamba kila mwaka wanapokutana na wadau hao wawe na mijadala yenye majibu ya utatuzi wa changamoto zao.

Naye Mbunge wa Kahama Mjini, Mhe. Jumanne Kishimba akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara walioshiriki mkutano huo, alisema wafanyabiashara wengi hukimbilia huduma za BRELA ili kupata huduma za mikopo kutoka taasisi za fedha na kupata zabuni ingawa wengi hawaelewi tafsiri za kisheria za kampuni.

Aliishauri BRELA kuzitafsiri kwa lugha nyepesi ili kuepusha migogoro inayotokana na uelewa hafifu wa sheria hizo.



*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa wakifuatilia mawasilisho kutoka kwa wawezeshaji wakati wa Mkutano wa Wadau wa BRELA.*

Awali katika hotuba yake, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw Godfrey Nyaisa, alisema kuna sheria zinzosimamiwa na BRELA ambazo zimepitwa na wakati na kwamba Taasisi yake ipo kwenye hatua za maboresho ya sheria kama vile Sheria ya Taifa ya usajili wa Leseni za Viwanda ya mwaka 1967, Sheria ya Hataza ya Mwaka 1987, Sheria ya Miliki Bunifu ya Mwaka 1986, sheria ya leseni za biashara ya mwaka 1972 na Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2002 ili ziendane na mabadiliko ya kiteknolojia na ukuaji wa sekta ya biashara.

> "Mkutano huu uwe ni sehemu ya kupokea maoni ya Watanzania




*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji na Mbunge wa Jimbo la Kahama Mjini, Mhe. Jumanne Kishimba, wakiwa katika picha ya pamoja na wakurugenzi wa Bodi ya Ushauri ya BRELA baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Wadau uliofanyika Oktoba 27, 2023, Mlimani City, Dar es Salaam.*

Akihitimisha mkutano huo wa wadau, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya BRELA, Prof. Neema Mori, aliwaahidi wadau kuwa Bodi itasimamia Taasisi yake kuleta urahisi wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki na itaendelea na michakato ya kuwepo kwa sera na maboresho ya sheria bora zinazowezesha utoaji wa huduma bora na rafiki kwa jamii.

# BRELA, TAKUKURU wakubaliana kuharakisha taratibu za uchunguzi

**Na Theresa Chilambo**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) zimesaini hati ya makubaliano ya utendaji kazi ili kurahisisha na kuharakisha taratibu mbalimbali za uchunguzi bila kuathiri mamlaka na mipaka ya kiutendaji ya taasisi hizo mbili.

Hafla ya utiaji saini hati ya makubaliano iliongozwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Kamishina wa Polisi Salum Hamduni hapo Desemba 7, 2023 jijini Dar es Salaam.

Akizungumza mara baada ya utiaji saini makubaliano hayo, Bw Nyaisa alisema kuwa nia ni kuona uchunguzi unaenda haraka na kuhakikisha TAKUKURU wanapata taarifa zilizo sahihi kwa wakati.

“Katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku BRELA imekuwa ikipokea barua si chini ya sita kwa siku kutoka TAKUKURU zinazohitaji taarifa za usajili na leseni. Pia tumekuwa tukipokea wito unaowahitaji Maafisa wa BRELA kwa ajili ya mahojiano pamoja na kuhudhuria mahakamani kushuhudia taarifa za kumbukumbu hizo,” alisema Bw Nyaisa.

Naye Kamishina Hamduni alieleza kuwa Mkataba huo uliosainiwa unalenga katika kuweka nguvu na kurasimisha ushirikiano wa taasisi hizo mbili kwa maeneo yaliyoridhiwa na pande zote.

Maeneo hayo ni pamoja na kubadilishana taarifa za kiuchunguzi kwa lengo la kupata ushahidi utakowezesha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani, kuimarisha mfumo na utaratibu wa mafunzo kwa watumishi wa BRELA kuhusu



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna wa Polisi. Salum Rashid Hamduni wakisaini hati ya Makubalino ya Ushirikiano baina ya Taasisi hizo.*

dhana ya rushwa, madhara yake na namna watumishi hao wanavyoweza kupambana na changamoto hizo ndani ya BRELA.

Pia mkataba huo utasaidia kuimarisha ushirikiano katika kufanya utafiti na tathmini ya mifumo ya kiutendaji ndani ya BRELA kwa lengo la kubaini na kuziba mianya ya rushwa ndani ya taasisi.

"Kwa kutambua kuwa rushwa ni adui wa haki, utawala wa sheria, demokrasia na maendeleo, serikali imedhamiria kupambana na tatizo la rushwa kwa nguvu zote. Aidha, kwa kutambua kuwa mapambano dhidi ya rushwa hayawezi kufanikiwa bila ushiriki wa wadau, TAKUKURU kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 imekuwa ikishirikisha wadau mbalimbali ikiwemo kuingia nao mikataba ya ushirikiano," alisisitiza Kamishina Hamduni.

Aliongeza kuwa TAKUKURU itayazingatia Makubaliano haya ikiwa ni moja ya nyenzo muhimu katika kufikia Dira ya taasisi hiyo inayosema "Tanzania isiyokuwa na rushwa" kama ambavyo inabainishwa katika Mpango Mkakati wa TAKUKURU wa 2022/2023-2025/2026.

Aidha mnamo Julai 8 na 9, 2022, BRELA na TAKUKURU zilifanya kikao cha pamoja mkoani Morogoro chenye lengo la kupeana elimu ya kiutendaji ili kuleta uhusiano wenye tija katika kutimiza majukumu pamoja na kupeana taarifa mbalimbali kwa kuzingatia taratibu, kanuni na sheria.

Kutokana na kikao kazi hicho, ilionekana kuna umuhimu kwa taasisi hizo kuanzisha utaratibu wa kuwa na vikao vya pamoja kwa lengo la kupeana elimu na uelewa kuhusu utendaji kazi na mafanikio.

Hii ni pamoja na maboresho katika usajili wa kampuni na majina ya biashara, utunzaji wa rekodi na taratibu za kufuata baada ya usajili, kubadilishana uzoefu pamoja na kubainisha changamoto mbalimbali ili kupata ufumbuzi wa pamoja kwa manufaa ya taasisi hizo na taifa kwa ujumla.




*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa akimkabidhi shajala ya BRELA Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna wa Polisi, Salum Rashid Hamduni baada ya hafla fupi ya kusaini Makubalino ya Ushirikiano (MOU), baina ya Taasisi hizo.*

# Muarobaini wa takwimu za viwanda waja



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA (katikati) Bw, Godfrey Nyaisa na Mtendaji Mkuu wa TIRDO Prof. Mkumbukwa Mtambo (kulia) wakiwa katika kikao cha kujadili kuhusu mfumo wa takwimu za viwanda nchini walipokutana Oktoba 5, 2023 katika Ofisi za BRELA, Dar es Salaam.*

**Na Christina Njovu**

Menejimenti ya Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) na wataalam wa Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) wamejadili suala la kuanzishwa kwa mfumo wa takwimu za viwanda katika kikao kilichofanyika Oktoba 5, 2023, katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mkuu wa TIRDO Prof. Mkumbukwa Mtambo alikiambia kikao hicho kwamba lengo la mfumo huo ni kuwa na kituo kimoja cha kupata takwimu za viwanda tofauti na ilivyo sasa.

“Hivi sasa takwimu za viwanda zinapatikana katika taasisi tofauti tofauti, mathalan taarifa za kiwanda kidogo zinapatikana SIDO, viwanda vikubwa zinapatikana BRELA na kutoka taasisi nyingine. Hivyo, uanzishwaji wa mfumo wa takwimu za viwanda utawezesha kuwa na kituo kimoja cha kupata taarifa za viwanda,” alisema.

Akitoa maelezo kuhusu mfumo huo, Afisa TEHAMA wa TIRDO, Bi. Elizabeth Mtegwa, alisema katika utekelezaji wa zoezi hilo TIRDO imeanza kupita mikoa mbalimbali nchini kukusanya takwimu za viwanda. Kwa kuanzia imepata takwimu za viwanda katika mikoa ya Pwani, Morogoro na Dar es Salaam.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alisema BRELA iko tayari kushirikiana na TIRDO katika kuhakikisha kuwa mfumo wa taarifa za viwanda unakamilika mapema iwezekanavyo.



*Mkurugenzi wa Leseni wa BRELA (kulia) Bw. Andrew Mkapa akifafanua jambo wakati wa kikao cha kujadili kuhusu mfumo wa takwimu za viwanda nchini walipokutana na uongozi wa TIRDO tarehe Oktoba5, 2023 katika Ofisi za BRELA, Dar es Salaam.*

# DC ahimiza wajasiriamali kurasimisha biashara

**Na Sheila Mfunami**

Wajasiriamali walioshiriki katika Maonesho ya Wiki ya Huduma za BRELA na wadau wake wametakiwa kutumia fursa hiyo kurasimisha biashara zao ili ziweze kukua.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Mhe. Hashim Komba alitoa wito huo Oktoba 24, 2023 wakati akifungua maonesho ya kwanza ya BRELA na wadau wake yaliyofanyika viwanja vya Mlimani City, jijini Dar es Salaam.

"Wito wangu kwenu Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) na wadau wengine wa maonesho haya ni kwamba tuhakikishe hawa wajasiriamali mbalimbali wanakua, hivyo wasaidiwe kwa kupatiwa elimu ili waweze kurasimisha biashara zao," alisema Mhe. Komba.

Alisema ili kuboresha zaidi maonesho haya BRELA iendelee kuyaandaa katika maeneo mengine yatakayowezesha wadau wengi zaidi kufika. Aliyataja maeneo yeye idadi kubwa ya wajasiriamali katika Wilaya ya Ubungo kuwa ni Mbezi na Manzese, ambayo yanastahili kupewa kipaumbele kwa kuwapatia elimu.

Pia aliitaka BRELA kuimarisha uhusiano na taasisi nyingine za Serikali, hususan Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Serikali za Mitaa ambazo ndizo zinazowakutanisha wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa.

Mhe. Komba alisema Maonesho ya BRELA pia yatumike kufanya tathmini ya huduma zinazotolewa sambamba na kuwa na madawati yanayowakutanisha wadau ili kupunguza watu wa kati (vishoka) ambao wamekuwa kikwazo kikubwa kwa wafanyabiashara.

"BRELA, Tume ya Ushindani (FCC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) shirikianeni katika utoaji wa elimu ili kudhibiti na kupambana na bidhaa bandia, kuthibitisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali na kuhakikisha wanafanya sajili mbalimbali na kupata leseni," alisema.



*Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Mhe. Hashim Komba akifungua Maonesho ya kwanza ya BRELA na Wadau wake kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.*

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa alisema Taasisi yake itaendelea kuwahamasisha wadau wake kurasimisha biashara zao kupitia majukwaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonesho.

Maonesho ya BRELA na wadau wake ambayo yalihitimishwa na Mkutano wa Wadau Oktoba 27, 2023 uliofanyika Ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam yalibeba kaulimbiu ya "Urasimishaji Biashara katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda".



*Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Hashim Komba (katikati) akikata utepe ikiwa ni ishara ya kufungua rasmi Maonesho ya BRELA na wadau wake yaliyofanyika Mlimani City jijini Dar es Salaam.*

# Kamati yajadili Itifaki za Miliki Ubunifu Afrika

**Na Lugano Mwakyombe**

Kamati ya Uratibu wa zoezi la kuridhiwa kwa Itifaki zinazosimamiwa na Shirika la Miliki Ubunifu Kanda ya Afrika (African Regional Intellectual Property Organization - ARIPO) ilikutana kujadili Itifaki zinazosimamiwa na chombo hicho.

Kikao hicho kilichoanza Oktoba 2, 2023 jijini Dar es Salaam kilimalizika Oktoba 4, 2023.

Katika kikao hicho maafisa kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) pamoja na wadau mbalimbali walijadili Itifaki zinazosimamiwa na ARIPO ili kupendekeza uwezekano wa Itifaki hizo kuridhiwa na nchi wanachama. Itifaki hizo ni pamoja na Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea, Itifaki ya Kampala ya Ulinzi wa Hiyari wa Hakimiliki na Hakishiriki, Itifaki ya Banjul ya Ulinzi wa Alama, Itifaki ya Madrid ya Ulinzi wa Alama inayosimamiwa na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani pamoja na Itifaki ya Ulinzi wa Haki za Miliki Ubunifu chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA).



*Maafisa wa BRELA na COSOTA wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa kikao cha kujadili Itifaki zinazosimamiwa na ARIPO kilichofanyika Oktoba 2, 2023 katika Ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam.*



*Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu kutoka BRELA, Bi. Loy Mhando akitoa ufafanuzi kuhusu Itifaki hizo zitakavyoongeza wigo katika kulinda kazi za wabunifu nchini.*

Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu wa BRELA, Bi. Loy Mhando akizungumza kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, alisema Itifaki hizo ambazo nchi ilizisaini kwa nyakati tofauti, zitaongeza wigo katika kulinda Bunifu na Hakimiliki za kazi za wabunifu.

Kazi hizo ni pamoja na kazi za sanaa, uandishi, uzalishaji, utaoji huduma, hakimiliki za aina mpya za mbegu za mimea na bunifu nyingine.

Katika kikao hicho, Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ilijadiliwa, ikihusisha ulinzi wa Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea kikanda.

Kamati pia ilipitia Itifaki ya Kampala ya Usajili wa Hiyari wa Hakimiliki na Haki Shiriki ambayo iliwasilishwa na Afisa COSOTA Bw. Prosper Massawe ambaye alielezea namna wasanii wanavyoweza kunufaika kupitia Itifaki hiyo.

Alisema kwamba Itifaki hiyo itasaidia wasanii kuongeza wigo katika umiliki wa kazi zao na pia kupunguza changamoto na kuwaongezea mapato yao binafsi na taifa kwa ujumla.

> Itifaki hizo ambazo nchi ilizisaini kwa nyakati tofauti, zitaongeza wigo katika kulinda Bunifu na Hakimiliki za kazi za wabunifu.

# Baraza la wafanyakazi latakiwa kusimamia utendaji kazi

**Na Roida Andusamile**

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa ambaye pia Mtendaji MKuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) amewataka wajumbe wa chombo hicho kuhakikisha wanasimamia ipasavyo utendaji kazi na nidhamu ya watumishi ili kuongeza tija.

Bw. Nyaisa, ambaye pia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, alitoa agizo hilo Oktoba 20, 2023 wakati akifungua Kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika mjini Morogoro.

Alisema kwa kuwa Baraza hilo ni chombo cha ushirikishaji wa watumishi na linaundwa na wajumbe kutoka Menejimenti, viongozi wa Chama cha Wafanyakazi (TUGHE) na wawakilishi wa watumishi kutoka idara mbalimbali, wajumbe hao wana wajibu wa kusimamia utendaji kazi na nidhamu ya watumishi ili kutoharibu taswira ya Taasisi.

Aidha, Bw. Nyaisa alisisitiza kuwa viongozi wa TUGHE wakiwa wajumbe wa Baraza wanapaswa kufuatilia maslahi ya wafanyakazi kwa kushirikiana na Menejimenti. Hivyo, wanapoona kuna jambo lolote ambalo haliendi sawa wanapaswa kutoa taarifa mapema.

"Siyo jambo jema kwa viongozi wa TUGHE kukaa kimya kwa mambo ambayo yako wazi na kusubiri Menejimenti ya Taasisi ndiyo ifuatilie," alisisitiza.

Alisema wajumbe wanapaswa kuwasilisha taarifa na changamoto wanazokumbana nazo watumishi ili ziweze kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi ili kuwanufaisha watumishi wote.

Akizungumzia umuhimu wa vikao vya Baraza, Bw. Nyaisa alisema vinasaidia kutatua changamoto za wafanyakazi kwa uwazi na kuondoa manung'uniko ambayo yanaweza kujitokeza.

Baraza la Wafanyakazi hukutana katika vikao visivyopungua viwili kwa mwaka kwa ajili ya kujadili masuala yote yanayowahusu watumishi na kuidhinisha mipango na bajeti ya Taasisi. Vile vile Baraza hukutana ili kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa malengo ya BRELA kwa mwaka husika wa fedha.



*Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi Bw. Godfrey Nyaisa akiwa na Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Bw. Abas Cothema wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa BRELA kilichofanyika Oktoba 20, 2023 mjini Morogoro.*

# Dkt. Biteko awahimza watumishi wa umma kufanya mazoezi

**Na Sheila Mfunami**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewahimiza watumishi walioshiriki michezo ya mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali na Mikoa (SHIMIWI) kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi ili kujenga afya zao.

Alitoa wito huo Oktoba 4, 2023, wakati akifungua Mashindano ya SHIMIWI 2023 yaliyoanza Septemba 27 2023 mjini Iringa.

"Nimefurahia maendeleo yenu katika michezo hii, lakini niwakumbushe viongozi kuhimiza watumishi kufanya mazoezi, kuandaa mechi za kirafiki ili kujiweka sawa kwa mashindano kama haya." alisisitiza Mhe. Dkt. Biteko.

Alisema ni vyema ofisi za Serikali kuwa na viwanja vya michezo pamoja na kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara kwa ajili ya kuimarisha afya zao.

Aliongeza kuwa ana imani na ushiriki wa timu zote katika michezo hiyo ingawa kuna kushinda na kushindwa, huku akiwatakia heri na ushindi katika michezo hiyo iliyoanza Septemba 27, 2023 na kuhitimishwa Oktoba 14.

Mashindano ya SHIMIWI kwa mwaka 2023 yenye kauli mbiu "Michezo mahala pa kazi huimarisha afya na kuongeza ufanisi." BRELA ilishiriki katika mashindani hayo katika mchezo wa mpira wa miguu na wa pete.



# BRELA yaiduwaza HAZINA

**Na Sheila Mfunami**

Timu ya mpira wa miguu ya wanaume ya BRELA iliibuka mshindi kwa kuifunga Hazina bao moja kwa bila katika pambano la michezo ya SHIMIWI lililofanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa mjini Iringa Septemba 29, 2023.

Nayo timu ya mpira wa pete ya BRELA iliichabanga timu ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi magoli 10-1 katika pambano lililofanyika viwanja vya Chuo cha Ruaha mjini Iringa.

Mashindano hayo yaliyoanza rasmi Septemba 29, 2023 yaliamsha ari kwa timu za BRELA zikiwa zimepania kuondoka na ushindi wa kishindo.

Mashindano ya michezo inayoandaliwa na SHIMIWI yanalenga katika kuimarisha afya za watumishi, kuongeza ufanisi mahala pa kazi na kuwajengea uhusiano mzuri baina yao.

Mashindano hayo ya wiki mbili yalishirikisha watumishi wa Serikali kutoka Wizara, Idara na Taasisi.

Kaulimbiu ya mashindano haya ilikuwa "***Michezo mahala pa kazi huimarisha afya na kuongeza ufanisi kazini***".

Mashindano yalifunguliwa rasmi Oktoba 4, 2023 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Dotto Biteko katika Uwanja wa Samora mjini Iringa.

Katika mashindano hayo BRELA ni timu pekee iliyoifunga HAZINA ambaye alikuwa bingwa mtetezi na mshindi wa mashindano hayo.

# BRELA yaigalagaza RAS Mara

**Na Sheila Mfunami**

Timu ya mpira wa pete ya ya BRELA) iliibuka mshindi baada ya kuiadhiri timu ya RAS Mara kwa magoli 25-3.

Timu hizo zilichuana Oktoba 2 katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Ruaha mjini Iringa.

Timu ya BRELA ilionesha ubabe wake ikiwa ni mchezo wa nne tangu kuanza kwa mashindano hayo Septemba 29, 2023.

Mashindano hayo yenye lengo la kuimarisha mahusiano mazuri kwa watumishi na kuimarisha afya za watumishi yalihitimishwa Oktoba 14, 2023 kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa.

# BRELA changia vifaa vya michezo

**Na Sheila Mfunami**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa msaada wa vifaa vya michezo truck suits jozi 25 pamoja na mipira mitano kwa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA) vitakavyotumiwa na timu ya netiboli Wanawake, Taifa Queens.

Akikabidhi vifaa hivyo Novemba 22, 2023, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bi. Loy Mhando alisema BRELA ni mdau mkubwa wa michezo, kwakuwa inatambua kuwa michezo ni afya, ni burudani pia kupitia michezo Taasisi inajitangaza na zaidi ya hapo michezo ni biashara hivyo kama Taasisi inayohusika na masuala ya urasimishaji biashara ina wajibu wa kushirikiana na wana michezo nchini.

"BRELA imekuwa ikishiriki katika michezo mbalimbali na kutoa misaada kwa wadau wa michezo ili kuhakikisha kuwa sekta ya michezo nchini inakuwa na kujipambanua kimataifa", amefafanua Bi. Mhando.

Aidha Bi. Mhando alisema msaada wa vifaa uliotolewa unaunga mkono jitihada za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuhamasisha ukuaji wa sekta ya michezo nchini.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa CHANETA, Bi. Rose Mkisi aliishukuru BRELA kwa msaada wa vifaa vya michezo kwa timu ya Taifa Queens.

"Tunaishukuru sana BRELA kwa msaada wa vifaa vya michezo na tunaahidi kupitia vifaa hivi vya michezo timu ya Netiboli itafuzu vyema katika michuano mbalimbali watakayoshiriki.

BRELA ilitoa msaada wa vifaa hivyo baada ya kupokea maombi kutoka CHANETA kuhusu uhitaji wa vifaa vya michezo vitakavyotumika katika mashindano mpira wa pete nchini Botswana.

Hafla hiyo ya makabidhiano ya vifaa vya michezo ilifanyika katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.



*Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu Bi. Loy Mhando akikabidhi vifaa vya michezo kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA kwa Katibu Mkuu wa CHANETA Bi. Rose Mkisi Novemba 22, 2023 katika Ofisi za Wakala jijini Dar es Salaam.*

# Wafanyabiashara watakiwa kuchangamkia fursa za BRELA

**Na Sheila Mfunami**

Wafanyabiashara wametakiwa kuchangamkia fursa kwa kurasimisha biashara zao BRELA ili wapate mafanikio.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo, Oktoba 25, 2023, alipotembelea Maonesho ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na wadau yaliyofanyika Mlimani City Jijini Dar es Salaam.

Mhe. Mpogolo alisema lengo la Maonesho ya BRELA ni kuhamasisha wadau kurasamisha biashara zao kwa wingi, hasa kwa kipindi ambacho taasisi hiyo imeandaa maonesho na kuzishirikisha taasisi nyingine za umma ili kutoa huduma mahali pamoja.

Alifafanua kuwa mfanyabiashara anaporasimisha biashara yake hutambulika na taasisi za fedha na kumwezesha kupata zabuni mbalimbali pamoja na kutambulika rasmi kisheria.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Mhe. Halima Bulembo, aliipongeza BRELA kwa kuandaa Maonesho yenye tija kwa wafanyabiashara na kwa ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Nimefurahishwa sana na huduma nzuri inayotolewa na BRELA, hivyo basi wafanyabiashara ambao bado hawajarasimisha biashara zao ni vyema wakafuata taratibu sahihi za kusajili," alisema.

Maonesho hayo ya siku tano ya Wiki ya Huduma za BRELA na wadau wake yaliyobeba kaulimbiu "*Urasimishaji Biashara katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda*" yalifunguliwa Oktoba 24, 2023 na kuhitimishwa Oktoba 27, 2023. Mkutano wa BRELA na Wadau wake uliofanyika katika Ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam na kufunguliwa na Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji.




*Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Halima Bulembo wakikabidhi cheti cha Usajili wa Jina la Biashara kwa mteja aliyesajili wakati wa Maonesho ya BRELA.*

## Watumishi BRELA, Tume ya Ushindani wapata mafunzo ya Miliki Ubunifu

**Na Lugano Mwakyombe**

Watumishi wa Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) na Tume ya Ushindani wameshiriki katika mafunzo ya siku mbili ya uchakataji wa maombi ya Usajili wa Alama za Biashara na Huduma kwa njia ya mtandao wakiungana na washiriki wengine wa hapa nchini na wengine kutoka Afrika Kusini, Nigeria na Kenya.

Mafunzo haya yaliandaliwa na Chama Cha Kimataifa Cha Alama za Biashara (International Trademark Association - INTA) chenye makao makuu jijini New York, Marekani, kwa lengo la kuwajengea uwezo wa masuala ya Miliki Ubunifu.

Mafunzo yalifanyika jijini Dar es Salaam kuanzia Novemba 6 hadi 7, 2023.

Akizungumzia Utatuzi wa Migogoro inayotokana na Ulinzi wa Miliki Ubunifu, Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu wa BRELA, Bi. Loy Mhando, alisema taasisi yake imekuwa ikisikiliza mashauri yanayotokana na pingamizi ya maombi ya Usajili wa Alama za Biashara au maombi ya kuondoa Alama za Biashara kwenye Daftari la Msajili.

Naye mwezeshaji wa mada ya Udhibiti wa Bidhaa Bandia, Bi. Hazel Okoth, kutoka Kenya alisema bidhaa hizo zinapaswa kudhibitiwa ili kuendelea kuwapa haki na kuwaongezea kipato wamiliki halali wa Alama za Biashara zinazotumika katika bidhaa husika.

# Waaswa kusajili Alama za Biashara kabla ya kuingiza bidhaa sokoni

**Na Theresa Chilambo**

Wafanyabiashara wanaozalisha bidhaa na kutoa huduma katika Wilaya ya Nyamagana Jijini Mwanza wametakiwa kusajili Alama za Biashara na Huduma Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) kabla ya kuingiza sokoni ili kujipatia ulinzi wa kisheria na kuhimili ushindani katika soko.

Wito huo ulitolewa Novemba 13, 2023 na Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Hataza kutoka BRELA, Bi. Neema Kitala, wakati wa mafunzo kwa wafanyabishara wanaozalisha bidhaa na kutoa huduma mbalimbali wa Wilaya ya Nyamagana.

Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Nyakahoja jijini Mwanza.

"Uzuri wa kusajili Alama ya Biashara na Huduma yako ni kukitambulisha kile unachokizalisha sokoni na faida kubwa utakayoipata ni bidhaa yako kutambulika na kuaminika katika masoko, bidhaa hiyo kuonekana halali na ya kipekee, na kukupa faida ya kupenya katika masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi," alisema Bi. Kitala.

Alisisitiza kuwa wafanyabiashara wasiposajili Alama za Biashara na Huduma zao, pindi wanapotambulisha biashara zao sokoni licha ya kupendwa na watumiaji, hazitakuwa na ulinzi wa kisheria. Hivyo, mtu mwingine anaweza akaiga, akasajili na kuingiza sokoni na kusababisha migogoro ambapo utatuzi wake hutumia muda na gharama kubwa.

Naye mfanyabiashara wa chakula cha mifugo wilayani humo, Bi. Wilhelmina Kubingwa, alisema mafunzo hayo yatamwezesha kusajili Alama ya Biashara anayotumia katika bidhaa zake. Aliongeza kuwa ili kuweza kushindana katika soko ni muhimu kuweka ulinzi wa bidhaa zake kwa kusajili Alama anayotumia.



*Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Hataza kutoka BRELA, Bi Neema Kitala, akitoa elimu ya sifa za Alama ya Biashara na Huduma kwa wazalishaji wa bidhaa na huduma wa Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza.*

Wakati huo huo, Afisa Sheria wa BRELA, Bw. Calvin Rwambongo, alisema kwamba Taasisi yake inasimamia Sheria za Miliki Ubunifu ambazo ni Sheria ya Alama za Biashara na Huduma na Sheria ya Hataza.

Bw. Rwambongo alisema kuwa Sheria ya Alama ya Biashara inalenga kuwalinda wazalishaji wa bidhaa na huduma wanaobuni alama, nembo, michoro, ishara mbalimbali kwa lengo la kutofautisha bidhaa zao wanapoingiza sokoni na Sheria ya Hataza ni haki ya kipekee ya ulinzi inayompa mbunifu wa bidhaa mpya au mchakato mpya unaolenga kutatua changamoto za kiufundi.

Aliongeza kuwa Sheria ya Alama za Biashara na Huduma iko wazi kwamba Alama inaposajiliwa



*Afisa Sheria kutoka BRELA, Bw. Calvin Rwambongo, akitoa elimu kwa wazalishaji wa bidhaa na huduma wa Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza kuhusu umuhimu wa kusajili Alama za Biashara na Huduma.*



*Wafanyabiashara wanaozalisha bidhaa na kutoa huduma mbalimbali wa Wilaya ya Nyamagana, jijini Mwanza, wakifuatilia kwa makini mafunzo ya umuhimu wa kusajili Alama za Biashara na Huduma.*

inazuia wengine kutumia Alama husika pasipo idhini ya yule aliyesajili. Hivyo inamtambua kwa kumpa ulinzi yule tu aliyesajili na itampa haki yake endapo mtu mwingine atatumia Alama kama hiyo na kuiingiza sokoni.

Rwambongo aliwashauri wazalishaji wa biashara na huduma kukimbilia BRELA kulinda haki zao na kutotumia Alama za Biashara na Huduma za watu wengine kwa kuwa athari yake ni kubwa ambayo inaweza kusababisha bidhaa zake kuteketezwa na kulipa fidia.

BRELA ilitoa mafunzo kwa wafanyabiashara kuhusu usajili wa Alama za Biashara na Huduma kuanzia Novemba 13 hadi 17, 2023 katika Wilaya za Nyamagana, Ilemela, Misungwi na Ukewere mkoani Mwanza.

# Aipongeza BRELA kuwanoa wafanyabiashara

**Na Theresa Chilambo**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imepongezwa kwa kuchukua hatua ya kuwanoa wafanyabiashara wa Mwanza kuhusu elimu ya Alama ya Biashara na Huduma kwa kuwa wengi huzalisha bidhaa na kuziingiza sokoni bila kujua umuhimu wa Sajili hizo.

Pongezi hizo zimetolewa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Bw. Balandya Elikana, alipotembelewa na Maafisa kutoka BRELA katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Novemba 14, 2023.

Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Hataza wa BRELA Bi. Neema Kitala, alimweleza kuwa Taasisi imedhamiria kuwajengea uwezo wazalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali kwa lengo la kuwalinda katika masoko yenye ushindani mkubwa ili waweze kuaminika na kuwaepusha kuingia kwenye migogoro.

Wakiongea kwa nyakati tofauti baada ya mafunzo ya usajili wa Alama za Biashara na Huduma wazalishaji wa bidhaa na huduma wa Wilaya ya Ilemela, Bi Fauzia



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza Bw. Balandya Elikana akiwa na maafisa wa BRELA walipomtembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Novemba 2023.*

Ibrahim ambaye ni Meneja wa Kampuni ya Joasamwe inayozalisha gundi ya karatasi, alisema kuwa walianza uzalishaji baada ya kusajili kampuni yao ila walikumbana na changamoto ya kutumia nguvu kubwa ya kutambulisha bidhaa yao sokoni.

"Bidhaa ya gundi ya karatasi inazalishwa ndani na nje ya nchi na bidhaa hizo zipo kwenye masoko mengi nchini ila kutokana na elimu tuliyopata tutachukua hatua ya haraka kusajili Alama yetu ya Biashara ili iweze kujulikana na kutofautishwa na washindani wetu kwa kuwa bidhaa yetu ni bora zaidi," alisema.

Mjasiriamali mwingine, Bw. Salum Ramadhani, alieleza kuwa changamoto kubwa ni kutokuwa na ufahamu wa usajili wa Alama za Biashara, yeye alijua usajili ni wa kampuni tu lakini kupitia mafunzo amepata ufahamu na atatengeneza alama za biashara ambazo zitakuwa na upekee na zenye kutambulisha bidhaa za kampuni yake.

Naye Bi. Salome Nyakwaka aliishukuru BRELA kwa kutoa elimu ya Alama za Biashara na Huduma kwa kuwa wengi walikuwa hawajui umuhimu wa kusajili alama zao na wengi wanazalisha bidhaa kwa kuweka alama zenye mfanano bila kufahamu athari ya kutumia alama hizo.

BRELA inasimamia sheria ya Miliki Ubunifu ambazo ni Sheria ya Alama za Biashara na Huduma na Sheria ya Hataza. Sheria ya Alama ya Biashara inalenga katika kuwalinda wazalishaji wa bidhaa na huduma wanaobuni alama, nembo, michoro, ishara mbalimbali kwa lengo la kutofautisha bidhaa zao wanapoingiza sokoni.

Aidha, Sheria ya Hataza ni haki ya kipekee ya ulinzi inayompa mbunifu wa bidhaa mpya au mchakato mpya unaolenga kutatua changamoto za kiufundi katika jamii.




*Wafanyabiashara wanaozalisha bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kutoka Wilaya ya Ilemela, wakisikiliza kwa makini Afisa Sheria kutoka BRELA, Bw. Calvin Rwambongo, alipokuwa akiwasilisha mada kuhusu umuhimu wa kusajili Alama ya Biashara na Huduma katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela jijini Mwanza.*

# Uelewa hafifu kikwazo cha usajili wa alama za biashara

**Na Mwandishi Wetu**

Baadhi ya wafanyabiashara wa Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza wameeleza kuwa kuingiliana kwa nembo za biashara sokoni, mlolongo mrefu wa kupata huduma ya usajili.

Wakizungumza Novemba 15, 2023 katika semina ya kuwajengea uelewa wa hatua za usajili wa Alama za Biashara na Huduma na hatua za Usajili wa Hataza kwa njia ya mtandao, wafanyabiashara hao wadogo na wa kati walitaja changamoto nyingine kuwa ni ukosefu wa elimu na ofisi za BRELA ngazi ya wilaya.

"Kuna haja kila mkoa au wilaya nchini wakawepo mawakala wa BRELA kwa lengo la kuongeza thamani, kuwarahisishia wafanyabiashara kufanya usajili ambapo kwa pamoja utasaidia kuongeza mapato ya Serikali na kupunguza changamoto hizo za wafanyabiashara," alisema Rashid Bashite, Katibu wa Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo wa Wilaya ya Misungwi

Katibu Msaidizi wa Mtandao wa Wanawake Wanaojishughulisha na Shughuli za Uvuvi Tanzania (TAWFA), Fatuma Katulla, aliiomba BRELA kuzidi kutoa elimu zaidi kwa wananchi na wafanyabiashara ili kila mtu awe na uelewa wa kutosha kuhusu urasimishaji biashara.

"Changamoto ambazo tunazipata kwanza ni kuingiliana kwa nembo na watu zaidi ya mmoja. Sasa unakuta bidhaa zinaleta shida mtu anahitaji bidhaa ya mtu fulani anaikosa kwa sababu ya nembo zinafanana na hazijasajiliwa," alisema Fatuma

Akizungumzia mafunzo hayo na changamoto hizo, Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Hataza BRELA, Neema Kitala, alisema taasisi hiyo imejipanga kutoa elimu ya usajili na urasilimishaji wa biashara katika mikoa yote nchini.

"Changamoto kubwa tunayokutana nayo ni wadau wetu kuomba ofisi za BRELA ziwe katika kila mkoa au wilaya kwani kwa sasa ofisi zetu zipo Dar es Salaam na Dodoma kwa hiyo hatuna ofisi katika mikoa mingine.

"Hivyo wadau wameshauri tuanzishe ili kuwasaidia kupata huduma kwa karibu zaidi kwahiyo tumelipokea na tutalipeleka kama ombi kutoka kwa wadau wetu ili kuanzishwa ofisi za kanda au ikiwezekana katika kila mkoa," alisema.

---

# Wagonjwa Ocean Road wapata msaada

**Na Njwaba Mwaijibe**

Wakala wa Usajili na Biashara na Leseni (BRELA), imetoa mahitaji mbalimbali kwa wagonjwa katika Hospitali ya Ocean Road jijini Dar es Salaam.

Akikabidhi msaada huo Novemba 3, 2023 kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu, Afisa Habari Mkuu wa BRELA, Bi. Christina Njovu, alisema kuwa Taasisi imekuwa ikitekeleza Sera ya Urejeshaji kwa Jamii kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa misaada kwa watu wenye uhitaji.

Alisema BRELA imekuwa ikishirikiana na jamii katika kutekeleza majukumu yake, na kwa hiyo itaendelea kutoa mahitaji mbalimbali kwa wenye uhitaji wakiwemo wagonjwa, kwa kutambua kuwa ni wadau muhimu katika urasimishaji wa biashara licha ya kukabiliwa na changamoto za kiafya.



*Maafisa wa BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na wawakilishi wa uongozi wa Hospitali ya Ocean Road mara baada ya kukabidhi mahitaji mbalimbali ya wagonjwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya BRELA ya kurejesha kwa Jamii.*

Pia aliziomba taasisi nyingine za umma na binafsi kuwa na utaratibu wa kutoa misaada kwa jamii ili kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwapatia wananchi huduma bora za afya.

Akizungumza kwa niaba ya Uongozi wa Hospitali ya Ocean Road, Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi Bi. Mary Haule aliishukuru BRELA kwa misaada hiyo kwa kuwa kuna wagonjwa mbalimbali wenye uhitaji kwenye hospitali hiyo.

Alizitaka taasisi nyingine kujitokeza kwa kutoa misaada ili wale wagonjwa wasio na ndugu wala jamaa wasaidiwe kupata mahitaji muhimu.

BRELA ilitoa misaada ya sabuni, miswaki, *diapers*, mafuta ya kupaka mwilini, dawa za meno na vitu vingine kwa ajili ya wagonjwa waliolazwa katika hospitali hiyo.

# Kamati ya Bunge yaimwagia sifa BRELA

**Na Roida Andusamile**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imeipongeza Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) kutokana na mabadiliko mbalimbali ya utendaji kazi yanayofanyika katika taasisi hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Deo Mwanyika alitoa pongezi hizo wakati wa semina maalum iliyoandaliwa na BRELA jijini Dodoma kuwaelimisha wajumbe wa Kamati kuhusu majukumu yanayofanywa na Taasisi hiyo.

Mhe. Mwanyika alisema changamoto zilizokuwepo awali za kiutendaji kwa sasa hazipo na matokeo yake BRELA inaendelea kufanya kazi kwa weledi na uadilifu.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe, akimwakilisha Waziri wa wizara hiyo, alisema elimu zaidi inapaswa kutolewa ili kuwa na uelewa mpana kuhusu majukumu yanayofanywa na BRELA.

“Kama mnavyoona kuna baadhi ya mambo mliyoyaeleza hapa Waheshimiwa Wabunge ndiyo wanayasikia hivyo semina hizi ni muhimu kufanyika mara kwa mara pamoja na kuwa na muda wa kutosha,” alieleza Mhe. Kigahe.

Awali Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw Godfrey Nyaisa, aliwaeleza wajumbe wa Kamati hiyo kuwa BRELA inaendelea kufanya maboresho mbalimbali ya kimifumo lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa wadau wanapata huduma za BRELA kwa urahisi zaidi.

Aliwahakikishia kuwa taarifa za wadau wote waliofanya sajili mbalimbali BRELA ambazo zinafanyika kwa njia ya mtandao zipo salama na Taasisi imekuwa ikishirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kuhakikisha kuwa mfumo unakuwa salama wakati wote.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo Mhe. Deodatus Mwanyika akifuatilia mawasilisho yaliyotolewa wakati wa semina kuhusu majukumu ya BRELA iliyofanyika Dodoma.*

Mjumbe wa Kamati, Mhe. Prof. Sospeter Muhongo, alitaka kufahamu kama BRELA ina mpango wowote wa kuwasaidia wabunifu waliojisajili BRELA kwa kuwatafutia masoko ya bunifu zao.

Akitoa ufafanuzi Msajili Msaidizi Mkuu wa BRELA Bw. Seka Kasera alisema Wizara ya Viwanda na Biashara ilianza mchakato wa kuwa na Sera ya Taifa ya Miliki Ubunifu ambapo maoni ya wadau yameshachukuliwa na sasa Sera hiyo iko hatua ya mwisho na itakapokamilika itawezesha kuwapatia masoko wabunifu mbalimbali ambao wamesajili bunifu zao BRELA.



*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb), akizungumza wakati wa semina ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu majukumu ya BRELA iliyofanyika Dodoma.*

> "Sheria iliyopo inatoa haki ya kipekee ya ulinzi kwa Bunifu mbalimbali

Alisema kuwa Sheria iliyopo sasa inaiwezesha BRELA kutoa linzi pekee kwa Bunifu mbalimbali.

"Sheria ya Miliki Ubunifu itakapofanyiwa marekebisho haitaishia kuweka ulinzi pekee bali itahakikisha kuwa bunifu hizo zinaingia sokoni ili wabunifu waweze kunufaika na bunifu zao," alifafanua Bw. Seka.

Mjumbe mwingine wa Kamati hiyo, Mhe. Abdul-Aziz Abood, alitaka kufahamu BRELA inashughulikiaje suala la ufanano wa majina ya Kampuni na ya Biashara wadau wanapopeleka maombi ya majina yanayofanana.

Akifafanua kuhusu hoja hiyo, Msajili Msaidizi wa BRELA Bi. Leticia Zavu, alisema vigezo vinavyotumika katika usajili wa Kampuni na Majina ya Biashara ni kutokuwa na ufanano wa matamshi na maandishi hivyo aliyesajiliwa awali ndiye hulindwa na kuendelea kutumia jina husika.

Katika semina hiyo BRELA iliwasilisha mada kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Kampuni, Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sheria ya Leseni za Biashara na Viwanda pamoja na Sheria ya Usajili wa Alama za Biashara na Huduma.



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akitoa ufafanuzi kuhusu Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao wakati wa semina ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu majukumu ya Wakala iliyofanyika Dodoma Novemba 9, 2023.*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge wakimsikiliza Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akitoa ufafanuzi kuhusu Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao wakati wa semina ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu majukumu ya Wakala iliyofanyika jijini Dodoma.*

**Nukuu:**

- "Tunaendelea kuboresha mifumo ya usajili ili kurahisisha upatikanaji wa huduma zetu." Bw. Godfrey Nyaisa
- "Toeni elimu kuhusu majukumu ya BRELA mara kwa mara ili kukuza uelewa wa wadau". Mhe. Exhaud Kigahe (Mb)
- "Ninawapongeza BRELA kwa kuboresha utendaji kazi." Mhe. Deodatus Mwanyika (Mb)





BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# Manyara wahamasishwa kurasimisha biashara

**Na Peter Tweve**

Maafisa wa Wakala wa Usajili na Leseni (BRELA) wamehamasisha vijana wa Mkoa wa Manyara pamoja na wadau wengine kurasimisha biashara, huku wakitoa usaidizi katika Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (*Online Registration System* – ORS na Dirisha la Taifa la Biashara), kwa wadau waliokwama kukamilisha sajili mbalimbali zinazotolewa na Taasisi hiyo.

Uhamasishaji huo ulifanyika katika Maonesho ya Wiki ya Vijana yaliyofanyika mkoani Manyara ambayo yalishirikisha wajasiriamali mbalimbali. Maonesho hayo yalihitimishwa Oktoba 14, 2023 sambamba na kilele cha mbio za Mwenge na kumbukizi ya kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Maonesho hayo yalikuwa na mwitikio mkubwa ambapo wadau wengi walifika katika banda la BRELA ili kupata huduma mbalimbali ambazo zilikuwa zikitolewa papo kwa papo.



*Afisa wa BRELA, Bi. Winifrida Gaudence (mwenye fulana nyeusi), akitoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA kwa wajasiriamali walioshiriki maonesho ya Wiki ya Vijana yaliyofanyika katika stendi ya zamani, Babati mkoani Manyara. Maonesho hayo yaliyofanyika kwa siku saba, maafisa wa BRELA pia walitoa usaidizi kwa wadau wenye changamoto katika Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS) na Dirisha la Taifa la Biashara (TNBP).*



# Utatuzi wa migogoro katika Miliki Ubunifu

**Na Lugano Mwakyombe**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeshiriki katika warsha ya siku mbili (2) ya uchakataji wa maombi ya Usajili wa Alama za Biashara na Huduma. Aidha, washiriki wa warsha hii ambao ni watumishi kutoka BRELA na Tume ya Ushindani walipata mafunzo kwa njia ya mtandao wakiwa wameungana na washiriki wengine ambao walikuwa ni baadhi ya Mawakili wa hapa nchini na washiriki kutoka Afrika Kusini, Nigeria na Kenya.

Mafunzo haya yaliandaliwa na Chama Cha Kimataifa Cha Alama za Biashara (International Trademark Association-INTA) chenye Makao yake Makuu New York, Marekani kwa lengo la kuwajengea uwezo watumishi wanaoshughulikia masuala ya Miliki Ubunifu. Mafunzo yalifanyika katika Ukumbi wa FCC, jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 6 Novemba, 2023 na kuhitimishwa tarehe 7 Novemba, 2023.

Akizungumza katika Warsha hiyo kuhusu Utatuzi wa Migogoro inayotokana na Ulinzi wa Miliki Ubunifu, Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu kutoka BRELA Bi. Loy Mhando alieleza kuwa BRELA katika utekelezaji wa majukumu yake, imekuwa ikisikiliza Mashauri yanayotokana na pingamizi ya maombi ya usajili wa Alama za Biashara au maombi ya kuondoa Alama za Biashara kwenye Daftari la Msajili.

Kwa upande wake mwezeshaji wa mada kuhusu Udhibiti wa Bidhaa Bandia Bi. Hazel Okoth kutoka nchini Kenya, alisema bidhaa bandia zinapaswa kudhibitiwa ili kuendelea kuwapa haki na kuwaongezea kipato wamiliki halali wa Alama za Biashara zinazotumika katika bidhaa husika.



*Washiriki kutoka BRELA na FCC wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa warsha ya uchakataji wa maombi ya Usajili wa Alama za Biashara na Huduma iliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa FCC, Dar es Salaam.*

HABARI PICHA



*Mjasiriamali Bi. Atupakisye Mwaisaka (kulia) akikabidhiwa cheti cha usajili wa Jina la Biashara na Afisa wa BRELA Bw. Amon Mongela wakati wa maonesho ya Wiki ya Huduma za BRELA na wadau yaliyofanyika mwishoni mwa Oktoba, 2023, Mlimani City, Dar es Salaam.*



*Baadhi ya washiriki wa maonesho ya kwanza ya BRELA na wadau wake wakimsikiliza mgeni rasmi wakati wa uzinduzi wa maonesho hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Mlimani City, Dar es Salaam Oktoba 24, 2023.*




*Msaidizi wa Usajili Mwandamizi kutoka BRELA, Bw. Nassoro Mtavu (kulia), akimkabidhi cheti cha usajili wa Jina la Biashara Bi. Najma Nurudin (kushoto), mara baada ya kukamilisha taratibu za usajili katika banda la BRELA, Oktoba 23, 2023 wakati wa Maonesho ya Nne ya SIDO Kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Sabasaba mjini Njombe.*



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt Ashatu Kijaji (Mb), Oktoba, 2023 alifanya ziara ya kikazi katika Ofisi za BRELA, jijini Dar es Salaam na kufanya mazungumzo na Afisa Mtendaji Mkuu, Bw. Godfrey Nyaisa pamoja na baadhi ya maafisa waandamizi wa BRELA, Oktoba 6, 2023..*

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## FAHAMU KUHUSU MFUMO WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA



Mfumo wa kupokea taarifa za Wamiliki Wanufaika ni mfumo unaojitegemea kutoka kwenye mfumo wa **Online Registration System (ORS)** hivyo kampuni ambazo zina maombi yanayoendelea kwenye ORS bado zinaweza kuwasilisha taarifa zake za Wamiliki Manufaa kupitia link ya **https://bo.brela.go.tz**

**"TUNAIPA UHAI WA KISHERIA BIASHARA YAKO"**




*Watumishi wa BRELA na wanafunzi kutoka Chuo cha Diplomasia cha Dkt. Salim Ahmed Salim wakiwa katika picha ya pamoja tayari kwa kuwahudumia washiriki wa Mkutano wa wadau wa BRELA uliofanyika Oktoba 27, 2023 Mlimani City, Dar es Salaam.*



*Afisa wa BRELA Bw. Peter Paul Geay (kushoto) akimhudumia mteja aliyefika kusajili Jina la Biashara wakati wa Maonesho ya Kitaifa ya SIDO yaliyofanyika mwezi Oktoba, 2023 mjini Njombe*

HABARI PICHA



*Baadhi ya wanawake wajasiriamali wakisikiliza mada zilizowasilishwa wakati wa Jukwaa la Uwezeshaji wanawake kiuchumi Tanzania lililofanyika Desemba 19, 2023 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam. BRELA ilishiriki kutoa elimu katika jukwaa hilo.*



*Afisa wa BRELA, Bw. Stanslaus Kigosi, akitoa huduma za papo kwa papo katika Maonesho ya Utalii ya Swahili International Tourism Expo 2023, yaliyofanyika Oktoba, 2023 katika Ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (Mb), akipata maelezo kuhusu ushiriki wa BRELA katika maonesho ya Viwanda kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Bi Roida Andusamile. Kushoto ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe(Mb). Prof. Mkenda alitembelea banda la BRELA Oktoba 4, 2023 katika maonesho hayo yaliyofanyika ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam.*



*Afisa wa BRELA, Bw. Ndeyanka Mbowe (aliyesimama kushoto), akimhudumia Bw. Robert Makule aliyetembelea banda la BRELA Oktoba 4, 2023 wakati wa Maonesho ya Viwanda (TIMEXPO) yaliyoandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania - CTI) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) katika ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini Dar es Salaam.*






*Baadhi ya washiriki wa Warsha ya Uhamasishaji kuhusu dhana ya Wamiliki Manufaa wakisikiliza hotuba ya ufunguzi iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Mhe. Jabir Shekimweri kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Desemba 5, 2023 katika Hoteli ya Rafiki jijini Dodoma*



*Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri (katikati) akisalimiana na Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili Kanda ya Dodoma, Wakili Mary Munisi (kulia) wakati wa ufunguzi wa Warsha ya uhamasishaji kuhusu utekelezaji wa kanuni za dhana ya Wamiliki Manufaa wa Kampuni na Majina ya Biashara kwa wadau wa BRELA Desemba 5, 2023 mkoani Dodoma, kushoto ni Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Kampuni, Bw. Harvey Kombe.*



*Baadhi ya wadau wakiwa wamesimama kuwaombea waliofariki na waathirika wa mafuriko yaliyotokea wilaya ya Hanang, mkoani Manyara wakati wa Warsha ya uhamasishaji wa dhana ya Wamiliki Manufaa iliyoandaliwa na BRELA Desemba, 5 2023 jijini Dodoma.*

HABARI PICHA



*Baadhi ya washiriki wa warsha ya wadau wa utekelezaji wa dhana ya Wamiliki Manufaa wa Kampuni na Majina ya Biashara wakimsikiliza Mgeni Rasmi Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri wakati wa ufunguzi wa warsha hiyo Desemba 5, 2023 katika Hoteli ya Rafiki jijini Dodoma.*



*Watumishi wa BRELA wakishirki Mkutano wa wanawake kuhusu fursa za mkataba wa Eneo Huru la Biashara Bara la Afrika uliofanyika tarehe 6 Desemba, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam.*




*Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri (aliyekaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa warsha ya uhamasishaji wadau kuhusu dhana ya Wamiliki manufaa wa Kampuni iliyofanyika katika Hoteli ya Rafiki Dodoma*



*Afisa wa BRELA Bw. Nassoro Mtamvu, akitoa huduma katika banda la Taaasisi hiyo Oktoba 23, 2023 katika maonesho ya nne ya kitaifa yaliyoandaliwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), katika Uwanja wa Sabasaba mjini Njombe.*




*Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa maafisa wa BRELA (hawapo pichani), alipotembelea banda hilo kabla ya kufunga Kongamano la 14 la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi, nje ya Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa (AICC) Desemba 14, 2023 jijini Arusha. Mhe. Kikwete alitoa pongezi kwa BRELA kwa kutoa huduma bora kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS).*

# Fahamu misingi ya sheria ya kampuni

**Na Meinrad T. Rweyemamu**

Sheria ya Kampuni ilitokana na hitaji la kuwa na soko huria (free market economy) ambayo ilitokana na mageuzi ya kiuchumi ya kuelekea katika mfumo wa kibepari. Sheria ya Kampuni inaweka mpangilio ambao unatumika kuleta pamoja vyanzo vya uzalishaji kwa kuweka mipangilio miwili, ya kwanza ni kuanzisha kampuni ambayo ni chombo kinachotumika katika uzalishaji au ufanyaji biashara na pili ni kuleta soko la mtaji ambapo fedha inakusanywa kwa ajili ya kuwezesha mchakato wa uzalishaji au ufanyaji biashara.

Katika soko la mitaji, umma hualikwa kuingiza mtaji kwenye kampuni kwa kununua dhamana (securities) pale ambapo Kampuni inaweka dhamana hizo sokoni. Hizi zinaweza kuwa katika mfumo wa mtaji wa hisa au mkopo kwa kampuni. Dhamana huwapa wamiliki haki dhidi ya Kampuni. Kwa upande wa hisa, mara nyingi hutoa haki kwa wamiliki kwenye mali za kampuni zitakazosalia wakati kampuni inapofungwa baada ya kulipa madeni yenye dhamana na wadeni wengine.

Wanahisa wa kampuni wanayo mamlaka ya kuteua uongozi wa Kampuni pamoja na Wakurugenzi. Uongozi wa kampuni ndio wenye jukumu la kununua nyenzo za uzalishaji ambazo hujumuisha mali na wafanyakazi. Baada ya kuanza uzalishaji kampuni huuza bidhaa au huduma inazozalisha na kupata fedha au mali nyingine ya thamani. Endapo baada ya kipindi fulani cha uzalishaji kampuni inapata zaidi kutokana na shughuli zake kuliko kiasi cha mtaji kilichowekezwa, faida inakuwa imetengenezwa kwa wanahisa wake.

Faida inayopatikana mara nyingi kuna utaratibu wa kuhakikisha inawanufaisha wanahisa iwe kwa njia ya kuwapatia gawio au kwa kupandisha thamani ya hisa kwenye soko kwa kuzingatia ukweli kwamba thamani au mali za kampuni zimeongezeka. Pia ingawa ni kwa nadra sana, faida inaweza kugawiwa kwa wanahisa




*Afisa wa BRELA, Neema Nyadzi (kulia) akitoa huduma saidizi kwa mdau mwenye changamoto ya usajili kupitia mfumo.*




*Mtumishi wa BRELA Bw. Farid Hoza (kulia) akitoa huduma kwa wateja waliofika kwenye banda la Wakala katika uwanja wa Amri Abeid, Arusha wakati wa Maonesho ya Taasisi za Kifedha yaliyofanyika Novemba, 2023.*

wakati wa kufunga kampuni. Mara nyingi kufungwa kwa kampuni huashiria mwisho wa kampuni kujiendesha kwa faida kwamba mali za kampuni haziwezi tena kulipa wadeni wake.

Sheria ya Kampuni imeainisha aina mbalimbali za kampuni kama chombo cha ufanyaji biashara. Kampuni zinaweza kuingizwa katika makundi mawili, kampuni binafsi na kampuni za umma (Private and Public Companies) zenye ukomo wa hisa na zilizoundwa kwa mujibu wa sheria. Pamoja na kwamba misingi ya kisheria ya usimamizi wa kampuni hizi ni ile ile tofauti kubwa baina ya kampuni binafsi na kampuni ya umma ni pamoja na utofauti wa majina ya mwisho, kampuni ya umma jina lake huishia na neno “public Limited company” kwa kifupi ‘plc’ wakati kampuni binafsi uishia na neno ‘limited’ kwa kifupi ‘ltd’; kampuni ya umma inaweza kuuza hisa zake kwa umma wakati kampuni binafsi haina uwezo huo; Kampuni ya umma haina ukomo wa wanahisa wakati kampuni binafsi haiwezi kuwa na wanahisa zaidi ya hamsini; Hisa za kampuni ya umma zinahamishika kirahisi wakati hisa za kampuni binafsi zina utaratibu maalum wa kuhamisha; kampuni ya umma inapaswa kuhakikisha kwamba Katibu wake ana sifa zilizoainishwa kwenye sheria wakati kampuni binafsi haina kigezo hicho;

Kampuni kwa mujibu wa sheria zimepewa utu ili kuzitofautisha na wamiliki wake, kwa mfano mali ya kampuni inamilikiwa na kampuni na si wanahisa endapo Kampuni itanunua gari, gari hilo linakuwa katika jina la kampuni na sio jina la wanahisa. Kampuni pia zinaleta dhana ya ukomo wa madai (limited liability) ambapo hasara ambayo wanahisa wanaweza kuingia wao binafsi kutokana na shughuli za kampuni ni kiasi walichowekeza au kiasi walichoahidi kuwekeza kwenye kampuni. Hivyo kampuni inapofilisika, wanahisa wake hawatakiwi kulipia hasara nje ya kiwango walichowekeza au kuahidi kuwekeza. Kwa msingi huo dhana ya ukomo wa madai ina jukumu kubwa la kuwezesha kampuni kupata mtaji kwa kuwawezesha watu binafsi kuwekeza kiasi kidogo kidogo kwenye hisa za kampuni bila kuhatarisha mali zao binafsi pale kampuni inapofilisika.

Suala kubwa katika hii dhana ni utofautishaji wa kampuni na wamiliki wake, kwa msingi kwamba uwepo wa kampuni unaweka ukomo wa madai dhidi ya wanahisa na ndio maana mara nyingi tumeona kampuni inafilisika lakini wamiliki hawafilisiki. Bila hii dhana hakuna sababu ya kuwa na Sheria ya Kampuni. Huu ndio utofauti ulipo baina ya kampuni na jina la biashara. Watu wengi wamekuwa wakisajili jina la biashara na kufikiri kwamba wana ulinzi kama ilivyo kwa wamiliki wa kampuni zenye ukomo wa madai. Jina la Biashara halina utu wa kisheria na halimtofautishi mmiliki na jina hilo, endapo kunakuwepo na madai basi mmiliki wa jina la biashara anawajibika binafsi kulipa madai hayo na mali zake au fedha zake zinaweza kukamatwa kulipa madai.

# Miliki Ubunifu nyenzo muhimu ya kukuza biashara

**Na Stanislaus Kigosi**

Miliki Ubunifu ni dhana inayotambulika kwa kuangalia haki zinazomilikiwa na mbunifu katika kazi zake, kama ambavyo imekuwa ikifafanuliwa na kuelezewa katika mazingira tofauti tofauti. Miliki Ubunifu ni mali isiyoshikika lakini inakidhi vigezo vyote vya mali nyingine tunazozitambua kama majengo na mashamba.

Hivyo, Miliki Ubunifu hulindwa kwa sheria mbalimbali kama Sheria ya Usajili wa Hataza, Sheria ya Alama za Biashara na Huduma na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki. Hizi ni baadhi tu ya sheria katika mfumo wa sheria za Miliki Ubunifu.

Miliki Ubunifu imekuwa nyenzo muhimu sana katika kukuza na kuendeleza biashara. Maendeleo ya uchumi na ukuaji wa biashara vinategemea sana Miliki Ubunifu na mifumo madhubuti ya ulinzi wa haki za Miliki Ubunifu. Katika ufanyaji wa biashara na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali tumezungukwa na Miliki Ubunifu ambao wakati mwingine tunashindwa kutambua thamani yake. Lakini ubunifu huo ndiyo kila siku tunautumia katika kufanya majukumu yetu ikiwemo biashara. Maeneo mengi ya biashara kama migahawa na maduka au kumbi za burudani, muziki imekuwa ni nyenzo muhimu sana kuchangamsha maeneo hayo na hata kuwa kivutio cha wateja wanaofuata huduma na bidhaa katika maeneo hayo.

Hivyo, ni katika mazingira ya aina hii, kwa sasa hapa Tanzania, muziki umekuwa ni miongoni mwa biashara kubwa na yenye kuingiza kipato kikubwa sana kwa wanamuziki. Lakini bahati mbaya kwa aina nyingine ya Miliki Ubunifu haijafikia hatua kubwa katika kuifanya kuwa ni biashara na pia nyenzo muhimu ya kukuza biashara.

Mifumo madhubuti ya ulinzi na usimamizi wa kazi za Miliki Ubunifu kama vile alama za biashara, hataza, hakimiliki huchochea maendeleo ya kijamii na uchumi. Uvumbuzi wa madawa na vifaa tiba ni matokeo kuwa na mifumo imara ya kulinda uvumbuzi wa wengine, lakini pia ni matokeo ya kuthamini uvumbuzi unaofanywa na wabunifu ambao wameamua kwa jitihada zao kutatu changamoto zinazoisumbua jamii kama vile magonjwa.

Ulinzi wa Miliki Ubunifu husaidia kukuza teknolojia katika maeneo mbalimbali duniani. Shirika la Biashara Ulimwenguni (WTO) kwa kutambua kuwa Miliki Ubunifu ni moja wapo ya kichocheo muhimu



*Wajasiriamali wakionesha bidhaa zao walizobuni katika maonesho ya wiki ya huduma za BRELA na wadau wake, yaliyofanyika Mlimani City, Oktoba 2023*



katika kukuza na kuendeleza biashara ulimwenguni, liliamua kuja na Mkataba wa Kimataifa katika Masuala ya Biashara na Miliki Ubunifu (TRIPs Agreement).

Vipaumbele vikuu vinavyosima`miwa katika Mkataba huu ni ulinzi wa haki za wabunifu katika Miliki Ubunifu katika biashara za kimataifa, na kusambaza teknolojia kwa mataifa yanayoendelea na mataifa masikini ulimwenguni.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba WTO walitambua kwamba bila ulinzi wa Miliki Ubunifu, ni vigumu sana biashara ya kimataifa kukua na kuweza kuleta tija kwa maendeo ya kijamii na kiuchumi kwa watu ulimwenguni.

Shirika la Biashara Ulimwenguni wameyapa mataifa yaliyoendelea jukumu la kuhakikisha wanatoa ruzuku kwa taasisi zao ili kupeleka teknolojia katika mataifa yanayoendelea na mataifa masikini.

Pia, Miliki Ubunifu huongeza thamani katika bidhaa na huduma zinazotolewa na wafanyabiashara. Matumizi ya alama za jumuiya katika bidhaa au huduma huwa ni ishara ya ithibati kuwa bidhaa au huduma husika inafaa kwa matumizi au ni bidhaa halali. Hii huongeza imani kwa walaji. Alama za kijamii katika bidhaa na huduma hutumika kuonesha kuwa bidhaa fulani imetokea eneo fulani. Na yeyote ambaye atatumia alama hiyo bila ridhaa na kama bidhaa husika haina uhusiano na ile alama ya jamii, basi anakuwa amevunja sheria na pia hatua za kisheria huweza kuchukuliwa kwa namna ambavyo itaonekana kuwa inafaa ili kuendelea kuwalinda wamiliki wa alama husika lakini pia kuwalinda walaji.

Alama za jamii na alama za ithibati ambazo hutumika kwenye biashara na huduma hujenga



*Mjasiriamali mbunifu wa mavazi akimhudumia mteja aliyetembelea bandani kwake wakati wa maonesho ya Wiki ya Huduma za BRELA.*

mahusiano ya kuaminiana kati ya mlaji na mzalishaji wa bidhaa na huduma husika. Mahusiano haya ya kuaminiana huwa ni kichocheo muhimu katika kukuza na kuendeleza biashara husika.

Matumizi ya Miliki Ubunifu katika biashara pia huweza kutumika kama mojawapo ya mbinu ya kuwadhibiti washindani kwenye soko hasa wale wenye nia ovu ya kughushi bidhaa. Kuna wakati ambapo mfanyabiashara anaweza kuwa amefanikiwa kuitumia alama yake katika soko na imefanikiwa kupata wateja wengi na imeweza kujijengea heshima kubwa katika jamii na sokoni kwa ujumla. Lakini, anaweza kutokea mshindani wa kibiashara akaamua kuisajili ile alama ambayo mwenye nayo hajaisajili kwaajili ya kupata ulinzi wa kisheria. Hii inakuwa ni njia rahisi ya kumuondoa mmiliki halali wa alama hiyo kwenye soko. Sababu ni kwamba sheria inamtambua yule tu aliyeisajili alama hiyo kuwa ndiye mmiliki halali wa alama husika ya biashara. Ni muhimu sana kwa wazalishaji wa bidhaa na huduma kuhakikisha kuwa alama zao ambazo zinawatambulisha kwa walaji zimesajiliwa na kupata ulinzi wa kisheria.

Kampuni zote kubwa ulimwenguni hujenga taswira yake kwa walaji kwa kutumia alama za biashara na huduma. Kwao, ulinzi wa alama zao za biashara na huduma huwa ni kipaumbele cha kwanza kabla hata ya bidhaa au huduma zao. Maana wanajua kwamba wakishalinda taswira yao kupitia alama zao za biashara na huduma, itawawia rahisi hata kuzalisha bidhaa na huduma bora kwani tayari walaji wana mapokeo chanya ya alama zao za biashara ambazo wamezilinda kwa kufanya usajili kwenye masoko yao.

Lengo kuu la kulinda alama zao ni kuhakikisha washindani wao kibiashara hawatumii alama zao kuwaondoa kwenye soko ambalo tayari wameliingia na kufanya biashara pia wakiwa wameshapata imani ya walaji wao. Kujenga imani ya walaji wa bidhaa na huduma ni kazi ngumu sana, lakini mshindani kibiashara anaweza kuiharibu taswira ya biashara ya mwingine kirahisi sana hasa kama alama hiyo anajua haijasajiliwa na haina ulinzi unaotambulika kisheria.

Ni vyema kwa wafanyabiashara kuona umuhimu wa kutumia Miliki Ubunifu kama mojawapo ya zana zao za kimkakati katika kukuza biashara zao. Miliki Ubunifu huwapa fursa ya kuwa vinara na kulishika eneo ambalo wanafanya biashara au uwekezaji wao. Miliki Ubunifu ndiyo kitu pekee kinachoweza kujenga mahusiano ya kudumu kati ya mfanyabiashara, mzalishaji bidhaa au mtumiaji wa huduma fulani pamoja na wateja wake.

# Umuhimu wa kampuni kuzingatia maadili ya ufanyaji biashara

<u>**Na Meinrad T, Rweyemamu**</u>

Kampuni ni chombo ambacho huundwa kisheria kwa lengo la kuwezesha wamiliki kufanya biashara na pia kutambulika kisheria kwa lengo la kuiwezesha kuingia mikataba na makubaliano mbalimbali. Kampuni inapaswa kuzingatia maadili ya ufanyaji biashara katika shughuli zake kama ambavyo mtu binafsi anavyopaswa kufanya kwa uwazi na uwajibikaji kwa kila shughuli inayofanyika.

Mbali na suala la uzingatiaji wa maadili ya biashara ndio njia sahihi ya kuchukua, kuna faida nyingine nyingi kwa Kampuni ambayo inatoa kipaumbele kwa suala hili. Uadilifu katika biashara unaongeza heshima ya kampuni ambayo upelekea kampuni kuvutia na kutunza wateja wake, kuongeza utiifu (loyalty) wa watumishi wake hivyo kuwezesha kampuni kuvutia uwekezaji zaidi. Suala la uadilifu katika ufanyaji biashara wa kampuni linakwenda sambamba na matokeo mazuri ya kifedha.

Hivi sasa kuna dhana mpya ya uadilifu katika Kampuni, hapo awali Kampuni zilitoa kipaumbele kwa maslahi ya wanahisa peke yake, lengo likiwa ni kuhakikisha wanahisa wanapata faida kutokana na uwekezaji walioufanya. Hivi karibuni kumekuwa na dhana mpya ya kuzitaka kampuni pamoja na kusimamia maslahi ya wanahisa wake, zizingatie pia maslahi ya wadau wengine hususan jamii. Dhana hii inazitaka Kampuni kuzingatia masuala ya Mazingira, Jamii na Utawala (Environment, Social and Governance – ESG) wakati wa kufanya maamuzi ya ununuzi au uwekezaji wa kampuni. Dhana ya ESG nitaifafanua katika Makala nyingine kwani ni dhana ambayo inahitaji ufanunuzi wa kipekee. Yote haya ni kuhakikisha kwamba Kampuni inaendeshwa katika misingi ya uadilifu, uwazi na uwajibikaji.

Kutokana na msingi huo, wakati wa usajili wa Kampuni, Wakurugenzi husaini kiapo cha maadili (Intergrity Pledge) wakiahidi kwamba Kampuni wanayounda itaendeshwa kwa misingi ya sheria na kuzingatia misingi ya ufanyaji na uendeshaji biashara ambayo ni pamoja na uadilifu, kutekeleza miadi ya kibiashara watakayoingia, kutojiingiza katika vitendo visivyozingatia ushindani wa soko na kuwa wawazi katika shughuli zake. Kampuni pamoja na kuzingatia maslahi ya wanahisa wake, inapaswa pia kuzingatia maslahi ya wateja wake wakati wa kufanya biashara na kutojihusisha na vitendo vya kitapeli au vitendo vyo vyote vya kijinai.

Hivi karibuni, kumekuwa na malalamiko dhidi ya baadhi ya Kampuni zilizosajiliwa hapa nchini kujihusisha katika vitendo vya kitapeli ambapo kampuni hizo zimekuwa zikiingia mikataba ya kuuza bidhaa au huduma kwa wateja walioko nje na ndani ya nchi na kuwataka wateja hao kulipia bidhaa hizo na baada ya hapo kampuni hizo zimekuwa hazitekelezi mikataba hiyo kwa kutoa sababu zisizo na mashiko na kutorejesha fedha walizopokea. Hali hii si tu inaathiri mhusika aliyedhulumiwa bali inasababisha Kampuni za kitanzania kuwa na rekodi mbaya kimataifa; Kuchafua taswira nzuri ya Taifa letu katika masoko ya kimataifa; Kudumaza jitihada za Serikali kutafuta masoko ya nje ya nchi; Kupunguza mapato ya fedha za kigeni na kupunguza ajira.

Sheria ya Kampuni, Sura 212 kifungu cha 400A (1)(b) kinampatia Msajili wa Kampuni mamlaka baada ya kujiridhisha kwamba Kampuni inajihusisha na vitendo vya kijinai kuifuta kampuni husika kwenye Daftari la Kampuni. Lengo la mamlaka haya ni kuhakikisha kwamba Kampuni hazitumiki kama mwamvuli wa kufanya uovu au utapeli. Pia kuhakikisha kwamba Daftari la Kampuni linakuwa na kampuni ambazo zinawajibika katika biashara zake.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 181 cha Sheria ya Kampuni, Sura 212 Wakurugenzi wa Kampuni wamepewa jukumu la kuelekeza na kusimamia uendeshaji shughuli na biashara za kampuni. Pia vifungu vya 182, 184 na 185 vinaelekeza kwamba Wakurugenzi wa Kampuni katika kutekeleza majukumu yao watafanya hivyo kwa uadilifu, kwa nia njema na kwa lengo la kutekeleza hitaji halali kama inavyompasa mtu yeyote aliyepo katika nafasi ya Mkurugenzi.

Kutokana na hali hiyo ni muhimu Wakurugenzi wa Kampuni kuhakikisha kampuni wanazosimamia hazijihusishi na vitendo vya kijinai kwani vitendo hivyo vinaweza kusababisha hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao kwa malalamiko ya kiutapeli ambayo wamefanya wakiwa kama Wakurugenzi wa Kampuni.

Wakurugenzi na Wamiliki wa Kampuni watumie kampuni zao kwa malengo halali ya kibiashara kama yalivyobainishwa kwenye Sheria ya Kampuni, Sura 212. Uadilifu katika Biashara za kampuni ni kuhakikisha kwamba nia na matendo ya kampuni yanakwenda sambamba, kuhakikisha kwamba mahusiano ya Kampuni na wateja wake, wafanyakazi, wazabuni, wawekezaji na Mamlaka za Udhibiti yanazingatia nia na malengo ya kufungua Kampuni. Kampuni ni chombo cha kufanya biashara (business vehicle) hivyo maamuzi na mipango yote ya kampuni lazima ijielekeze katika kufanya biashara na si vinginevyo.

# Watumishi wa BRELA watakiwa kujikinga dhidi ya magonjwa


**Na Roida Andusamile**

Maafisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) wametakiwa kuzingatia kanuni za afya ili kujiepusha na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

Wito huo ulietolewa na wataalam wa afya wakati wa mafunzo yaliyotolewa kwa watumishi wa BRELA kuhusu UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahala pa kazi pamoja na elimu juu ya Afya ya Akili yaliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Taifa Cha Utalii, Dar es Salaam, Novemba 18, 2023.

Akizungumzia Afya ya Akili, Daktari Bingwa Mwandamizi wa fani hiyo kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dkt. Frank Masao, alisema kwa kuwa afya ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili na kijamii, hivyo afya njema ni pamoja na kuwa na afya ya akili.

Dkt. Masao alisema changamoto ya Afya ya Akili inaweza kudhibitiwa, hivyo watumishi wanatakiwa kuangalia mienendo ya maisha yao ya kila siku ili kuepuka msongo unaotokana na matokeo, shinikizo, mazingira magumu na hisia za mvutano.



*Daktari Bingwa wa Afya ya Akili, Dkt. Frank Masao, kutoka Hospitali ya Taifa akieleza umuhimu wa kupata ushauri wa kitabibu kwa mtu mwenye changamoto ya afya ya akili wakati wa mafunzo ya afya kwa watumishi wa BRELA.*

Dkt Masao alifafanua kuwa changamoto ya Afya ya Akili inatokea mtu anapokabiliwa na msongo kuliko uwezo wake, hivyo inapotokea hali hiyo mwenye changamoto asisite kufika hospitali kwa ajili ya kupata tiba na ushauri wa kitabibu ili kurejea katika hali ya kawaida.

Pia alisisitiza juu ya kuepuka matumizi ya vilevi kupindukia na tabia zingine hatarishi ambazo husababisha baadhi ya watu kupata changamoto ya Afya ya Akili na kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Daktari Bingwa wa magonjwa yasiyoambukizwa, Dkt. Richard Murihano, alieleza namna ambavyo watumishi wanaweza kuepuka kupata magonjwa hayo kwa kuzingatia lishe bora na mpangilio sahihi wa chakula.

Aidha, watumishi wa BRELA walikumbushwa kuhusu umuhimu wa kufanya mazoezi, angalau



*Mtumishi wa BRELA Bw. Ndeyanka Mbowe akipata moja ya vipimo vya afya wakati wa mafunzo ya afya kwa watumishi wa BRELA.*

HABARI

mara tatu kwa wiki ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji wa BRELA Bw. Daimon Kisyombe alisema kuwa Taasisi imeandaa mafunzo hayo ili watumishi wawe na afya njema wakati wote.

“Taasisi ina watumishi wengi vijana ambao wana tabia nyingi hatarishi ikiwa ni pamoja na ulaji usiozingatia kanuni za afya, hivyo ni muhimu kuwajengea ufahamu kuhusu masuala ya afya,” alifafanua.


Alisema azma na dhamira ya Serikali ni kupambana na UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukizwa, hivyo katika Mpango Mkakati ya Taasisi wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 suala hili limepewa kipaumbele, lengo likiwa ni kumlinda mtumishi na familia kuepuka hasara kwa Taifa.

Mbali na kupata elimu, watumishi hao pia walipata fursa ya kupima afya zao ikiwa ni pamoja na VVU, kisukari, shinikizo la damu pamoja na uzito.

BRELA imejiwekea utaratibu wa kuendesha mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wake kuhusu masuala mbalimbali, ikiwemo afya, kwa lengo la kuwajengea uwezo na uelewa kwa ajili ya ustawi wa watumishi.

BRELA

Pata taarifa zaidi kuhusu huduma zetu, na jihudumie mwenyewe kupitia link ya **https://ors.brela.go.tz**





*Dkt. Richard Murihano akifafanua kuhusu athari za magonjwa yasiyoambukizwa wakati wa mafunzo ya Afya kwa watumishi wa BRELA.*



*Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji wa BRELA, Bw. Daimon Nathani Kisyombe, akitoa neno la ukaribisho wakati akifungua mafunzo ya afya kwa watumishi.*



*Baadhi ya watumishi wa BRELA wakisikiliza wataalam wa afya wakati wa mafunzo kuhusu magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza yaliyofanyika Ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Utalii jijini Dar es Salaam.*



# Tanzania yashiriki Mkutano wa 47 wa Miliki Ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa 47 wa Shirika la Miliki Ubunifu Afrika (ARIPO) uliojadili taarifa ya mwaka pamoja na kupitisha mpango kazi wa mwaka 2024.




*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa akiwa na Mwakilishi kutoka Uganda katika Mkutano wa 47 wa Shirika la Miliki Ubunifu Kanda ya Afrika, iliyofanyika Gaborone Botswana.*

Washiriki wa Mkutano huo wa siku nne (4) uliofanyika Gaborone Botswana ni Wakuu wa Ofisi za Miliki Ubunifu kutoka nchi wanachama wa ARIPO, ambapo kwa upande wa Tanzania Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa aliongoza msafara wa Tanzania kwa kuambatana na Maafisa wa BRELA Bw. Seka Kasera na Bw. Alex Mashamba na upande wa Zanzibar ukiwakilishwa na Bw. Mustafa Haji kutoka Wakala Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA).

Mkutano huo wa siku nne (4) uliohudhuriwa na nchi wanachama 22 za Afrika ulifunguliwa rasmi tarehe 20 Novemba, 2023 na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Botswana Mhe. Mmusi Kgafela na kufuatiwa na Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa nchi wanachama wa ARIPO.

Katika mkutano huo ARIPO iliwasilisha taarifa ya utendaji kazi ya mwaka kwa wanachama ambayo ilijadiliwa na wanachama na kuipitisha na hatimaye kuwasilisha mpango kazi kwa mwaka 2024.



*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na maafisa alioambatana nao kutoka Tanzania nje ya ukumbi ulikofanyika Mkutano wa 47 wa Shirika la Miliki Ubunifu Kanda ya Afrika (ARIPO), Gaborone Botswana. Kutoka kushoto ni Bw. Mustapha Haji kutoka Wakala wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA), Bw. Alex Mashamba (wa pili kutoka kulia) na Bw. Seka Kasera (kulia) kutoka BRELA.*

HABARI

# Nchi wanachama ARIPO zatakiwa kuongeza nguvu kwenye Miliki Ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Botswana Mhe, Dkt Mokgweetsi Eric Masisi amewataka Mawaziri kutoka nchi wanachama wa Shirika la Miliki Ubunifu Kanda ya Afrika (ARIPO) kuhakikisha kuwa wanaongeza nguvu kwenye Miliki Ubunifu badala ya kutegemea Rasilimali pekee. Rais Masisi alitoa rai hiyo tarehe 24 Novemba, 2023 wakati akifungua Mkutano wa 19 wa Baraza la Mawaziri wa nchi wanachama wa ARIPO uliofanyika Gaborone Botswana.

Alisisitiza kuwa muda umefika kwa nchi za Afrika kuwekeza kwenye maarifa na ubunifu na siyo kutegemea rasilimali tu na kutolea mfano kuwa katika kipindi cha Uviko 19 nchi za Afrika zilikuja na bunifu nyingi zikiwa ni pamoja na dawa na vifaa kinga, hivyo bunifu kama hizo zinapaswa kuendelea.

Mhe. Rais pia aliwataka Mawaziri kuongeza bajeti zao kwenye masuala ya Miliki Ubunifu. Katika mkutano huo Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa alimwakilisha Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji.

Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulimchagua Mhe. Mmusi Kgafela, Waziri wa Biashara na Viwanda wa Botswana kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa ARIPO kwa kipindi cha miaka miwili. Mkutano huo wa siku mbili wa Baraza la Mawaziri hufanyika kila baada ya miaka miwili, mkutano uliopita ulifanyika Victoria Fall Zimbabwe mwaka 2021.




*Waziri wa Sheria na Katiba wa Uganda Bw. Nobert Mao (kulia) wakijadiliana jambo na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa (katikati) huku Msajili Mkuu kutoka Taasisi ya Usajili Uganda, Bi. Mercy Kainobwisho (kushoto) akifuatilia, wakati wa Mkutano wa 19 wa Baraza la Mawaziri wa nchi wanachama wa ARIPO unaofanyika Gaberone, Botswana.*

# BRELA yatoa elimu kwa wajasiriamali wanawake Dar es Salaam

**Na Njwaba Mwaijibe**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa elimu kwa wajasiriamali wanawake kuhusu huduma zinazotolewa na Taasisi pamoja na kuwahamasisha kurasimisha biashara zao ili kukua kibiashara.

Elimu hiyo ilitolewa na Msajili Msaidizi wa BRELA, Bi. Leticia Zavu Januari 27, 2023 kwenye semina ya wajasiriamali wanawake illiyofanyika katika ukumbi wa Ngome Holding House, jijini Dar es Salaam.

Bi. Zavu alieleza kuwa ili waweze kukua kibiashara na kutambulika na taasisi mbalimbali zikiwemo za kifedha ni muhimu kurasimisha biashara zao BRELA, kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS).

Pia aliongeza kwa kuwaeleza kuwa urasimishaji wa biashara utawawezesha kukua kutoka hatua moja kwenda nyingine, ikiwa ni pamoja na kuaminika zaidi kwa wateja sambamba na kuingia ubia na wafanyabiashara wengine.

Bi. Zavu alihitimisha kwa kuwaasa kuwa mafunzo hayo yakawawezeshe kuwa mabalozi wa BRELA ili elimu waliyoipata iwafikie wadau wengi zaidi.

Semina hiyo iliandaliwa na Zalisha Burudisha Nasi (ZBN) Entertainment kwa lengo kuwakutanisha wajasiriamali hao na kuzishirikisha taasisi mbalimbali zinazoweza kuwaendeleza kibiashara.




*Afisa Usajili wa BRELA Bi. Leticia Zavu akitoaa mada kuhusu huduma zitolewazo na BRELA wakati wa semina ya wajasiriamali wanawake iliyofanyika kwenye ukumbi wa Ngome Holdings House, Dar es Salaam.*

# Yatakiwa kuzifikia wilaya zote Arusha



**Na Roida Andusamile**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Bw. Missaile Mussa ameitaka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kuhakikisha elimu ya Miliki Ubunifu inawafikia wananchi katika wilaya zote za mkoa huo waweze kunufaika na ubunifu wao na kufanya biashara zao bila kikwazo chochote.

Akizungumza na maafisa kutoka BRELA waliofika kujitambulisha ofisini kwake kabla ya kuanza mafunzo kuhusu Miliki Ubunifu kwa wafanyabiashara wa Halmashauri za Jiji la Arusha, Meru na Longido, Bw. Mussa alisema: “elimu ya Miliki Ubunifu inapaswa kutolewa katika halmashauri zote zilizopo mkoani humo. Wakati mwingine mjipange kufika katika wilaya za Loliondo, Monduli na Karatu ambazo hamtazifikia kwa sasa.” alisisitiza Bw. Mussa.

Awali Afisa wa BRELA Bi. Julieth Kiwelu alimhakikishia Katibu Tawala huyo kuwa awamu ya kwanza BRELA itawafikia wafanyabiashara katika halmashauri tatu na awamu itakayofuata wilaya zilizobaki zitafikiwa.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha wafanyabiashara wote wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya Miliki Ubunifu na hatimaye kusajili Alama za Biashara na Huduma pamoja na Bunifu zao.

“Mfanyabiashara ama mvumbuzi anaposajili Alama ya Biashara na Huduma pamoja na uvumbuzi wake anakuwa amelindwa kisheria, hivyo kuna manufaa yanayotokana na usajili wa Alama za Biashara na Huduma au Uvumbuzi,” alifafanua Bi. Kiwelu.

Maafisa wa BRELA walikuwa mkoani Arusha kwa siku tano kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara kuhusu Miliki Ubunifu ambayo yalijikita katika kuhamasisha usajili wa Alama za biashara, huduma pamoja na utoaji wa Hataza.

Mafunzo hayo ni mwendelezo wa jitihada zinazofanywa na BRELA za kutoa elimu kwa wadau ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi.

HABARI

# Elimu ya Miliki Ubunifu ifundishwe kuanzia shule za msingi-Wadau

**Na Roida Andusamile**

Washiriki wa mafunzo ya Miliki Ubunifu katika Halmashauri ya Longido wamependekeza kwamba ili idadi ya wavumbuzi Tanzania iongezeke, elimu ya Miliki Ubunifu haina budi kutolewa kuanzia ngazi ya shule za msingi ili kuwaandaa wanafunzi kuwa wavumbuzi wakiwa bado wadogo.



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo kuhusu umuhimu wa usajili wa Alama za Biashara na Huduma yaliyofanyika wilayani Longido Novemba 30, 2023, wakimsikiliza Afisa wa BRELA Bw. Benedickson Byamanyilwowa (hayupo pichani)*

Akichangia mada baada ya wasilisho kuhusu umuhimu wa kusajili vumbuzi mbalimbali lililotolewa Novemba 30, 2023 na Afisa wa Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Benedickson Byamanyilwowa, mfanyabiashara Bw. Elisante Mwasha alisema elimu ya Miliki Ubunifu ni muhimu kufundishwa kuanzia ngazi ya shule za msingi ili kuwajengea uelewa wa kutosha na hatimaye kuzalisha wavumbuzi wengi nchini na kuzisajili vumbuzi hizo BRELA.

“Elimu mliyotupatia leo ni nzuri sana lakini naona kama imechelewa na endapo ningekuwa na elimu hii muda mrefu, mbali na biashara ninazofanya ningeweza kuvumbua vitu mbalimbali na kunufaika na uvumbuzi wangu,” alisema Bw. Mwasha.

Awali Bw. Byamanyilwowa aliwaeleza washiriki hao kuwa pamoja na kwamba BRELA imekuwa ikitoa elimu na kuhamasisha wadau kusajili vumbuzi zao, mwamko wa sajili hizo bado ni mdogo.

Kutokana na hali hiyo, BRELA imejikita katika kutoa elimu kuhusu Miliki Ubunifu katika vyuo vya kati na vyuo vikuu ili kukuza uelewa wa vijana kuhusu masuala ya Miliki Ubunifu ambayo wakiizingatia itawanufaisha kwa kuwapatia ajira.

“Hakuna maisha bila hataza, vumbuzi inaongeza ajira, inamwezesha mvumbuzi kubaki katika ushindani ndani na nje ya nchi na zaidi inampa haki ya kipekee ya kumzuia mtu yoyote kutumia vumbuzi yake,” alieleza Bw. Byamanyilwowa.

Akielezea kuhusu vigezo vya uvumbuzi kama ilivyoanishwa katika Sheria inayolinda uvumbuzi sura 217, alisema uvumbuzi ni ule unaotatua changamoto katika jamii kwa kutoa suluhisho la changamoto hiyo au tatizo hilo, mfano mvumbuzi aliyevumbua miwani alilenga kutatua changamoto ya mtu mwenye tatizo la uoni hafifu wa kuona karibu au mbali, hivyo mvumbuzi huyo akatatua changamoto hiyo kwa kuvumbua miwani yenye lenzi za kuona karibu na kuona mbali.

Kisheria uvumbuzi lazima uwe ni mpya, uvumbuzi huo ukisajiliwa unalindwa kwa miaka 20 na mvumbuzi anachopaswa kufanya ni kuhuisha vumbuzi yake kwa kulipa shilingi 4,000/- kwa mwaka wa kwanza na baada hapo atatakiwa kuhuisha kila mwaka kwa gharama ya shilingi 1,000/-, huku gharama za awali za usajili na kupata cheti ikiwa ni shilingi 22,000/-.

Kwa upande wake Afisa Sheria wa BRELA Bw. Andrew Malesi akiwasilisha mada kuhusu umuhimu wa kusajili logo, alisema logo ni mali kama mali nyingine, hivyo endapo itasajiliwa inaweza kuuzwa au kutumiwa na mtu mwingine kwa makubaliano maalum na mmiliki wa logo husika.

Aliwaeleza kuwa matumizi ya logo ni kwa wafanyabiashara wote kuanzia wadogo, wa kati na wakubwa hivyo ni muhimu wakabuni logo za biashara zao na kuzisajili ili waweze kijitofautisha sokoni, kujitangaza na hata kutumiwa na mtu mwingine kwa makubaliano maalum na mmiliki wa logo husika.

BRELA ilikuwa mkoani Arusha kuanzia Novemba 27, 2023 kutoa elimu ya Miliki Ubunifu kwa wafanyabiashara ambapo elimu hiyo ilitolewa kwa zaidi ya wafanyabiashara 180 wa Arusha Jiji, Halmashauri ya Wilaya Arusha, Meru na Longido.

# Acheni kukwepa kusajili BRELA - Shekimweri

**Na Gloria Mbilimonywa**

Wafanyabiashara wametakiwa kuacha tabia ya kufanya biashara bila kusajili Majina ya Biashara na Kampuni zao na kukwepa kulipa kodi wakidhani wananufaika bila kujua kwamba wanakosa fursa mbalimbali za maendeleo ikiwemo mikopo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Mhe. Jabir Shekimweri Desemba 5, 2023 jijini Dodoma alipokuwa akifungua semina kuhusu dhana ya Wamiliki Manufaa wa Kampuni na Majina ya Biashara kwa mawakili, wahasibu, kampuni za ushauri wa biashara na wafanyabiashara.

"Kutokulipa kodi, kutokusajili kampuni kutokuwa na leseni, kufanya biashara kienyeji, unaweza ukaona ni ujanja lakini mwisho wa siku hutafanikiwa, itakunyima fursa ya kukopa, utakuwa na mapato makubwa mkononi wakati kwenye nyaraka, taarifa na kumbukumbu na rekodi za ulipaji wako wa kodi utakuwa umedanganya, kwa hiyo huwezi kupata mkopo na kubaki kuwa mlalamishi kuwa hupewi mkopo," alisema Mhe. Shekimweri.

Mhe. Shekimweri, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma katika ufunguzi wa warsha hiyo, aliwahimiza wafanyabiashara kufanya biashara katika mazingira rasmi kwa lengo la kupata mafanikio.

Aliwataka washiriki hao kutumia mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kuzielewa Sheria na Kanuni za Umiliki Manufaa katika kampuni na utaratibu wa kuwasilisha taarifa kwa msajili wa kampuni.

Naye Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, ambaye ni Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Kampuni, Bw. Harvey Kombe, alisema kuwa Taasisi itaendelea kukutana na wadau kwa lengo la kushauriana na kuelekezana kuhusiana na mabadiliko ya sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na marekebisho ya sheria ya makampuni sura namba 212 ya uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa.



*Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri akiwahutubia washiriki wa warsha ya uhamasishaji wa wadau wa BRELA kuhusu dhana ya Umiliki Manufaa. Kushoto kwake ni Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Kampuni Bw. Harvey Kombe na Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili Kanda ya Kati, Bi. Mary Munissi.*

Mwenyekiti wa Chama Cha Mawakili Kanda ya Kati Dodoma, Wakili Mary Munissi aliungana na kauli ya Mkuu wa Wilaya kwa kuwataka wateja wao kujenga tabia ya kuzingatia na kufuata sheria na kanuni za biashara za kusajili kampuni zao na kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Alitoa wito kwa mawakili kuacha tabia ya kuwakumbatia kwa kuwatetea wateja wao wanaokiuka taratibu, sheria na kanuni hizo, bali kinachotakiwa ni kuwaelimisha umuhimu wa kuzifuata bila shuruti.



*Baadhi ya washiriki wa warsha ya wadau wa utekelezaji wa dhana ya Wamiliki Manufaa wa Kampuni na Majina ya Biashara wakimsikiliza Mgeni Rasmi Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabir Shekimweri wakati wa ufunguzi wa warsha hiyo Desemba 5, 2023 katika Hoteli ya Rafiki jijini Dodoma*

# Watumishi wapya wapata mafunzo elekezi

**Na Sheila Mfunami**

Watumishi wapya wa Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) wameshiriki katika mafunzo yanayolenga kuwapatia maarifa na ujuzi utakaowasaidia katika utendaji kazi za Taasisi.

Mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku sita kuanzia Desemba na kuhitimishwa Desemba 11 katika Ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa Chuo na Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Dkt. Ernest Mabanesho, katika ufunguzi wa mafunzo hayo, aliipongeza BRELA kwa kutekeleza wajibu wao katika kutimiza takwa la kisheria ambalo linawataka watumishi wote wapya katika utumishi wa umma wapewe mafunzo mara tu wanaporipoti katika vituo vyao vya kazi.

Mkuu wa Chuo alieleza kuwa mada mbalimbali zitakazowasilishwa kwa watumishi hao kuwa ni pamoja na Maadili, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, Muundo wa Serikali na Uendeshaji wa Ofisi, Utunzaji wa Nyaraka na Kumbukumbu, Huduma bora kwa Mteja na masuala ya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza.

Mkuu huyo alisisitiza kuwa watumishi hao wanapaswa kuzingatia maadili na kanuni mbalimbali za Utumishi wa Umma.

"Maadili ni msingi muhimu wa utendaji bora wa kazi na tunatarajia kila mmoja wenu atazingatia maadili haya katika utumishi wenu. Sheria na kanuni za utumishi wa umma ni muhimu katika kuongoza matendo yetu na kuhakikisha uwajibikaji na uwazi katika utendaji wetu wa kazi," alifafanua Dkt. Mabanesho.



*Baadhi ya watumishi wa BRELA wakimsikiliza mkufunzi (hayupo pichani) kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma wakati wa mafunzo elekezi yaliyotolewa katika Chuo cha Utumishi wa Umma hapo Desemba 4 hadi 9, 2023.*



Aidha, aliwataka washiriki wa mafunzo haya kuwa makini wakati wote wa mafunzo kwani yatajumuisha sheria na taratibu za BRELA.

"Ni muhimu kufahamu na kuzingatia sheria na taratibu zetu ili kuhakikisha utendaji wa kazi unaofuata na kuzingatia miongozo, taratibu, kanuni na sheria," alisema Dkt. Mabanesho

Mafunzo hayo yalihudhuriwa na watumishi 56, ikiwa pamoja na watumishi 16 wa ajira za kudumu, watumishi nane (8) waliohamia BRELA, ajira za mkataba 25 na watumishi saba (7) wanaojitolea kutoka Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TAESA).

# Dkt. Mwigulu aimwagia sifa BRELA kwa huduma bora

**Na Sheila Mfunami**

Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba amesifu huduma bora zinazotolwa na Wakala kwa wananchi.

Alitoa sifa hizo Desemba 16, 2023 wakati alipotembelea banda la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) nje ya Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha lilipofanyika Kongamano la 14 la Mwaka la

Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

Alisema amefurahishwa na huduma nzuri inayotolewa na BRELA ambayo aliielezea kuwa itaongeza idadi kubwa ya wadau watakaorasimisha biashara zao.

“Nimefurahishwa sana na huduma nzuri inayotolewa na BRELA, hivyo wafanyabiashara na wawekezaji ambao bado hawajarasimisha biashara zao ni vyema wakafuata taratibu sahihi za kusajili,” alieleza.




*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Mchemba akitembelea banda la BRELA nje ya Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC), wakati wa Kongamano la 14 la mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.*

Aliwataka wananchi wa mkoa wa Arusha kuchangamkia fursa hiyo ya kurasimisha biashara zao na kufika katika banda la BRELA ili kupata huduma za urasimishaji.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alimhakikishia waziri huyo kuwa Taasisi itaendelea kutoa huduma bora wakati wote, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa wadau hawakumbani na vikwazo vya kibiashara.

Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi lilifunguliwa Desemba 12, 2023 na kuhitimishwa Desemba 14 jijini Arusha.




*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Mchemba (kushoto) akimkabidhi tuzo ya udhamini Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa wakati wa Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.*

> “Nimefurahishwa na huduma nzuri inayotolewa na BRELA

# Arusha wahamasishwa kurasimisha biashara



*Afisa Sheria wa BRELA Bw. Edward Magayane (kushoto) akiwahudumia wateja wakati wa Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi lililfanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa AICC jijini Arusha, Desemba 14, 2023.*

**Na Sheila Mfunami**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewataka wafanyabiashara ambao bado hawajarasimisha biashara zao kufanya hivyo ili kuepuka changamoto mbalimbali za kibiashara.

Wito huo ulitolewa Desemba 13, 2023 na Afisa Sheria wa taasisi hiyo Bw. Edward Magayane jijini Arusha lilikofanyika Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

Bw. Magayane alisema katika kipindi cha Kongamano hilo, maafisa wa BRELA walikuwa wanatoa mwongozo kwa wadau waliotembelea banda lao kuhusu Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS).

Aliongeza kuwa mfanyabiashara anaporasimisha biashara yake humuwezesha kupata fursa mbalimbali ikiwemo mikopo kutoka taasisi za fedha, kupata zabuni zinazotangazwa serikalini na nyinginezo.

"Tunatoa ushauri na elimu kwa wadau wanaotembelea banda letu na wanaotaka kusajili



kampuni na huduma nyingine wafike kwenye banda letu tutawapatia usaidizi," alisema Bw. Magayane. Kongamano hilo lililoanza Desemba 12 lilihitimishwa Desemba 14.

> " Mfanyabiashara anaporasimisha biashara yake, humuwezesha kupata fursa mbalimbali

## Wanafunzi wa MUM waelimishwa Urasimishaji Biashara

**Na. Njwaba Mwaijibe**

Wanafunzi wa Chuo kikuu Cha Kiislam Morogoro (MUM), wamepewa elimu juu ya huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ili kuwa na uelewa juu ya huduma zinazotolewa na umuhimu wake.

Wanafunzi hao walipata elimu hiyo Desemba 13, 2023 walipofanya ziara ya mafunzo katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Akiwalisha mada juu ya huduma zinazotolewa na BRELA kwa wanafuzi hao, Afisa kutoka Kurugenzi ya Kampuni na Majina ya Biashara, Bi. Maryglory Mmari alisema kuwa, huduma zinatolewa na Taasisi ni pamoja na Usajili wa Majina ya Biashara, Usajili wa Kampuni, Usajili wa Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Leseni za Biashara kundi "A", Utoaji wa Leseni za Viwanda na Utoaji wa Hataza.

Aidha, Bi. Mmari alieleza kuwa sajili mbalimbali za BRELA ni muhimu kwa wadau kuzizingatia kwa sababu huwezesha biashara kutambulika na mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupata dhamana ya kukopesheka katika taasisi za kifedha.

"Mkumbuke kuwa mfanyabiashara anaporasimisha biashara yake anakuwa na wigo mpana katika soko sambamba na kupata nafasi ya kushinda zabuni mbalimbali ambazo hushindanishwa," alifafanua Bi. Mmari.




*Mtumishi wa BRELA, Bi. Maryglory Mmari akizungumza na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro walipofanya ziara ya mafunzo katika Ofisi za BRELA .*

Aliongeza kuwa mfanyabiashara aliyesajili biashara yake ana haki ya kipekee kutumia, Jina la Biashara, Kampuni, Leseni au Alama iliyosajiliwa na kuwa na haki ya kuwashitaki watakaotumia bila ridhaa yake.

Kwa upande wake Afisa kutoka Kurugenzi ya Leseni, Bw. Paul Peter aliwaeleza wanafunzi hao kuwa mfanyabiashara yeyote anatakiwa kukata Leseni kwani ndiyo kibali kitakachomuwezesha kufanya biashara husika, hivyo wale wenye biashara yenye sura ya kitaifa na kimataifa wanatakiwa kuwa na Leseni ya Biashara Kundi "A" ambayo hutolewa na BRELA.

Akizungumza kuhusu Miliki Ubunifu Bw. Benedickson Byamanyilwowa, alisema kuwa kwakuwa Miliki Ubunifu ni zao la akili ni vyema wavumbuzi wakajua umuhimu wa kulinda vumbuzi zao kwani ni bidhaa zenye thamani.

Aliongeza kwa kusema kuwa Alama ya Biashara au Huduma na Uvumbuzi uliosajiliwa BRELA, unamuwezesha mmiliki kuingia ubia wa kibiashara na wadau wengine na kujipatia faida.

Wanafunzi hao pia walielezwa kuhusu mahitaji na hatua za usajili zinazohitajika katika kukamilisha usajili kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao (ORS).

Ziara ya wanafunzi hao katika Ofisi za BRELA ni mwendelezo wa Taasisi kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA ili kukuza uelewa wa wananchi.



*Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM) wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa BRELA baada ya kukamilisha ziara ya mafunzo katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.*

# BRELA yatoa elimu kwa wafanyabiashara Mbeya

**Na Njwaba Mwaijibe**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imefanya ukaguzi elimishi kwa kukutana na wafanyabiashara katika maeneo yao ya biashara jijini Mbeya, lengo likiwa ni kuhamasisha urasimishaji wa biashara.

Katika zoezi hilo lilioanza Desemba 18, 2023, maafisa wa BRELA walitembelea soko la Mwanjelwa na kukutana na wafanyabiashara mbalimbali ambao walielimishwa kuhusu huduma za Usajili wa Kampuni na Majina ya Biashara na taratibu nyingine za baada ya usajili ikiwemo uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa wa Kampuni.



*Mfanyabiashara wa soko la Mwanjelwa jijini Mbeya (katikati) akiwa na maafisa wa BRELA Bw. Jacob Mkuye na Bi. Mourine Kitinusa, alipotembelewa wakati wa zoezi la utoaji elimu ya urasimishaji biashara na uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa wa Kampuni, Desemba 18, 2023.*

Akizungumza na wafanyabiashara hao, Afisa Usajili wa BRELA Bw. Jacob Mkuye alisema lengo la ziara hiyo licha ya kutoa elimu ni fursa ya kutatua changamoto mbalimbali ambazo wadau wanakumbana nazo wakati wa kufanya sajili katika Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS).

Alisema kuwa pia watatoa usaidizi kwa wadau walioshindwa kuwasilisha taarifa za mwaka za Kampuni na kwa wale walioshindwa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa.

Bw. Mkuye alifafanua kuwa uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa wa Kampuni ni zoezi endelevu liloanza tangu mwaka 2021 ambapo kampuni zinapaswa kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa wake kwa Msajili wa Kampuni.

Siku ya kwanza ya zoezi hilo BRELA iliwatembelea wafanyabiashara wapatao 80.



*Afisa Usajili wa BRELA Bw. Jacob Mkuye akimsaidia mfanyabiashara kuwasilishaji taarifa za mwaka za kampuni yake alipotembelea soko la Mwanjelwa, jijini Mbeya.*



BRELA

Jihudumie mwenyewe kwa kupakua fomu kupitia link ya

**https://ors.brela.go.tz**

# BRELA Yatakiwa kuweka kambi Mbeya kuhamasisha urasimishaji biashara

**Na Njwaba Mwaijibe**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetakiwa kuweka kambi mkoani Mbeya ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara mkoani humo wanarasimisha biashara zao kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

Rai hiyo ilitolewa Desemba 22, 2023 na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya Bw. Rodrick Mpogoro alipofanya mazungumzo na maafisa wa BRELA walipomtembelea ofisini kwake. Maafisa hao walikuwa Mbeya kwa ajili kutoa elimu kwa wafanyabiashara ya urasimishaji biashara zao.

Bw. Mpogoro alisema kuwa Jiji la Mbeya linazidi kukua kibiashara na hivyo ni vyema BRELA ikaweka kambi ya kutoa elimu ya kurasimisha biashara kwa wafanyabiashara wa jiji hilo.

Aliahidi kwamba Mkoa wa Mbeya utawasilisha mwaliko BRELA ili ishiriki katika vikao maalum vya jiji na halmashauri na kuwawezesha watumishi wa mkoa huo kuwa na uelewa wa kufikisha shughuli za Taasisi hiyo kwa wananchi.

"Nilipata taarifa ya ujio wenu hapa; niwapongeze kwa zoezi hili ambalo mmeliendesha. Ninawaomba mfikishe ombi letu kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, kuwa tunawahitaji mrudi hapa na kuweka kambi, ili wafanyabiashara wengi zaidi wasajili biashara zao, " alisema Bw. Mpogoro.

Aliongeza kuwa wafanyabiashara wengi hawajasajili majina ya Biashara wala Kampuni kwa kuwa hawana elimu ya namna ya kutumia Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS).

Alisisitiza kuwa kwa kuweka kambi maalum itasaidia wadau na wafanyabiashara wengi kusajili.

Pia alisema ili kuongeza idadi ya wafanyabiashara waliorasimisha biashara zao, mkoa utatoa mialiko kwa BRELA kushiriki katika makongamano mbalimbali ili kuchochea elimu ya urasimishaji biashara.

Ziara elimishi ya BRELA iliyoanza Desemba 18 hadi 22, 2023 ilihamasisha uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa wa Kampuni sambamba na kutoa elimu ya urasimishaji wa biashara kupitia usajili wa Kampuni na Majina ya Biashara na kuwakumbusha kuwasilisha taarifa za mwaka kwa kampuni zilizosajiliwa pamoja na kulipia ada za utunzaji wa Majina ya Biashara.



*Watumishi wa BRELA wakiwa ofisini kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya Bw. Rodrick Mpogoro walipomtembelea ofisini kwake.*

# Uadilifu ni nyenzo ya tija kazini



*Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Vitengo wakimsikiliza Afisa Mtendaji Mkuu Bw. Godfrey Nyaisa (hayupo pichani) alipokuwa akitoa salamu za Sikukuu ya Krismas na Mwaka Mpya 2024.*

**Na Gloria Mbilimonywa**

Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa amewataka wafanyakazi kufanya kazi kwa uadilifu ili kuiletea Taasisi tija na heshima.

Akiwatakia wafanyakazi heri ya Krismasi na Mwaka Mpya alizungumza nao hapo Desemba 2023, kiongozi huyo alitilia mkazo masuala ya nidhamu na kuheshimu sheria za kazi.

"Nimeona nizungumze kidogo nanyi wafanyakazi wenzangu kabla hatujauanza Mwaka Mpya wa 2024 ni vyema tukazingatia nidhamu katika kazi ikiwa ni pamoja na kuwahi kazini na na kutumia muda wa kazi vizuri kwa kuchapa kazi," alisema Bw. Nyaisa.

Aliwakumbusha wafanyakazi wote kuzingatia suala la mahudhurio kazini kama Kanuni za kazi zinavyotamka kwa kuwepo mahali pa kazi muda wote badala ya utegaji na uzururaji.

Bw. Nyaisa pia aliitumia fursa hiyo kukata keki na kuwalisha baadhi ya watumishi ikiwa ni ishara ya kuwatakia heri katika msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka wa 2023 na mwanzo wa Mwaka Mpya wa 2024.





*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akiwalisha keki watumishi Bi. Sofia Mtunzi (kulia) na Bi. Aziza Omar Juma (kushoto) kwa niaba ya watumishi wengine kama ishara ya kuwatakia heri ya sikukuu za mwisho wa mwaka na Mwaka Mpya 2024. Tukio hilo lilifanyika katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam, Desemba 20, 2023*

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# A CALL FOR COMPANIES TO FILE ANNUAL RETURNS

The Registrar of Companies invites companies incorporated in Tanzania to file annual returns as required by the Companies Act, Cap 212.

**HOW TO FILE ANNUAL RETURNS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM**

1.Log in on the Online Registration System (ORS)
2. Select e-service
3. Select company
4. Select Filling of annual return (accounts)/update
5. Fill in Compliance number
6. Fill in Company's details
7. Upload form 128 with signed and dated consolidated form and the latest Audited Accounts
8. Select mode of payment (Mobile or Bank)
9. After payment the application will be received for review.

**Note:** Filing fee of an annual returns is TZS 22,000 if submitted on time. Delayed submission of an annual returns attracts a late filing fee of TZS 2,500 (compounded) per every month delayed or part thereo




BRELA House, Plot No.. 23
Sokoine Drive / Shaaban Robert
P.O. Box 9393, 11101, Dar es Salaam,
Tel: +255 22 2212800
E-mail: ceo@brela.go.tz • usajili@brela.go.tz
Web: www.brela.go.tz

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# INVITATION FOR FOREIGN COMPANIES TO FILE FINANCIAL STATEMENT



The Registrar of Companies call all foreign companies with registered branches in Tanzania to submit their Financial Statement as required by the Companies Act, Cap 212.

## HOW TO FILE FINANCIAL STATEMENTS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM

1.Log in on the Online Registration System (ORS)
2. Select e-service
3. Select company
4. Select Filling of annual return (accounts)/update
5. Fill in Compliance number
6. Fill in Company's details
7. Upload audited financial statement together with consolidated form
8. Click proceed button
9. An application will be received by Business Registration and Licensing Agency (BRELA) for review and process
10. After the review and processing of an application, an invoice will be sent to the customer for the payment of the required fee.

**Note:** Submission of financial statement costs USD 220.00 if submitted on time. Delayed submissions of financial statement are charged USD 25.00 (compounded) per every delayed month.




Jengo la BRELA, Kitalu Na. 20, Kiwanja Na. 23
Sokoine Drive / Mtaa wa Shaaban Robert
S.L.P 9393, 11101, Dar es Salaam, simu: +255 22 2212800
Barua Pepe: ceo@brela.go.tz • usajili@brela.go.tz
Tovuti: www.brela.go.tz

brela_tanzania | BRELA Tanzania | brela_tanzania | +255 (0) 735 331 003 | BRELA ONLINE TV